Alhamisi Agosti 20, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580315

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Mwanafunzi mahututi kwa madai kupigwa na mwalimu

UKURASA 5




UKURASA 11

# Presha yapanda, yashuka wagombea ubunge CCM

**HALMASHAURI**

Kuu kupitisha panga leo, waliokiuka maadili, watuhumiwa wa rushwa matumbo moto...

*Endelea uk. 2*



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli akiongoza kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**




## SERIKALI YAPOKEA GAWIO BIL. 15/- NMB

UKURASA 3

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Phillip Mpango (katikati), akipokea mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. bilioni 15.2 kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Ruth Zaipuna (kushoto), ambazo ni gawio kwa Serikali kutoka benki hiyo, jijini Dodoma jana. **PICHA: WFM**

## Ofisi nyingine ya CHADEMA yachomwa, nyaraka zateketea

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

MICHEZO BWALYA SASA AIONA CHIPOLOPOLO SIMBA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akishiriki kuteketeza zana haramu za uvuvi alipofanya ziara ya kushtukiza usiku katika mwalo wa Kagongo wilayani Mwanga, mkoani Kilimanjaro. Kushoto ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mwanga, Zebrin Lubuva na Ofisa Mfawidhi Kanda ya Pwani, West Mbemati. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Presha inapanda, inashuka wagombea ubunge CCM

**Na Waandishi Wetu**

PRESHA inapanda, presha inashuka. Ndivyo inavyoonekana kwa wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliotiania ya kugombea ubunge na uwakilishi katika majimbo na Viti Maalum kutokana na kubaki saa chache kutangazwa watakaopeperusha bendera za chama hicho kuwania nafasi hizo.

Kupanda huko na kushuka kwa presha kunatokana na kauli mbalimbali zilizotolewa na viongozi wakuu wa CCM, wakiwamo Rais John Magufuli, kuwa watafanya mambo ambayo hayakutarajiwa katika kupitisha wagombea kulingana na vigezo vilivyowekwa.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Bashiru Ally, pia alikoleza moto kuonyesha hawatakuwa na mswalie mtume baada ya kusema Jumatatu iliyopita kuwa mbivu na mbichi zitajulikana leo kwa waliotia nia kugombea ubunge na uwakilishi wakati Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM itakapokutana kupitia majina ya wagombea.

Bashiru alisema vikao vya juu vya chama kwa ajili ya mchakato huo vimeshaanza mchakato wa kuwachuja waliotoa nia, huku akiwataka wote waliojitokeza wakae majimboni ili wale watakaopitishwa wachukue fomu ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ngazi za majimbo kabla ya muda uliowekwa kumalizika.

**WATUHUMIWA RUSHWA**

Kabla na kuanza kwa mchakato wa kutafuta wagombea ubunge, uwakilishi na udiwani ndani ya CCM, viongozi hao wakuu walisikika wakisema watakaokiuka kanuni na maadili ya chama pamoja na kujihusisha na rushwa, hawatapitishwa.

Miongoni mwa mambo yaliyosisitizwa na viongozi hao ni pamoja na wanachama kutumia rushwa katika kuomba kuteuliwa nafasi wanazoomba. Jambo hilo liliripotiwa katika maeneo mbalimbali kwamba baadhi ya wanachama waliotia nia walikuwa wakitumia fedha kuwarubuni wapigakura.

Kutokana na madai hayo, huenda NEC ikatoka na uamuzi mgumu wa kuwafyeka wale wote waliotumia mlungula kushawishi wajumbe wawape kura za kutosha kabla ya kuteuliwa kuwanuia nafasi hizo. Viongozi wakuu hao pia walikemea kwa nguvu suala hilo kabla na wakati wa mchakato wa kura za maoni.

"Nafahamu kwenye uchaguzi huwa kuna mambo mengi, lakini jambo moja nalijua kwamba uchaguzi wa CCM unaongozwa na Katiba na Kanuni. Yale ambayo tumekatazwa yasifanywe," alisema Humphrey Polepole, Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi alipozungumza na waandishi wa habari Agosti 5, mwaka huu.

Polepole tayari walikuwa na taarifa za baadhi ya wanachama waliotia nia kuwa walitumia rushwa katika mchakato wa awali wa uchaguzi ndani ya chama hicho.

."Ningependa ifahamike na napenda kuwahakikishia Wana - CCM wote tuko vizuri sana, na wale wachache ambao wamejaribu na kutujaribu, tutawashangaza. Nasema tutawashangaza," alisema Polepole.

"Tunapokea taarifa nyingi, nasema kipindi hiki tutawashangaza watu. Waliodhani kwamba ni 'business as usual' (kufanya kazi kwa mazoea) inaendelea, tutawafundisha watu adabu kipindi hiki," aliongeza.

Naye Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ambaye ni mjumbe wa vikao vya juu vya uamuzi ndani ya chama, Agosti 8, mwaka huu, alisisitiza kuwa hawatakuwa na huruma na watu waliojihusisha na vitendo vya rushwa

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan alisema "Baadhi ya wagombea na mawakala kwa niaba ya wagombea hutoa rushwa ili wapigiwe kura, baadhi ya wapiga kura huomba kupokea rushwa ili kupigia chama fulani na matendo haya siyo ya kiungwana," alisema , wakati akizindua jengo la ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Mpwapwa.

Alisisitiza kuwa rushwa imekuwa mwiba katika kufanikisha uchaguzi huru na haki na kwamba CCM ilikuwa inaendelea na mchakato wa kuwachambua walioomba nafasi mbalimbali za uongozi na watakaobainika walijihusisha na vitendo hivyo watakatwa na kuenguliwa.

"Hii ni kwa sababu aliyetumia rushwa achaguliwe hatatumia muda wa uongozi wake kuwadumia wananchi ili wapate maendeleo bali kurejesha fedha alizozitoa na pengine apate zaidi," aliongeza.

**WALIOJIPITISHA**

Wanachama wengine ambao huenda wakakutana na panga la NEC ni wale waliodaiwa kujipitisha majimboni kabla ya wakati, hivyo kukiuka kanuni za chama. Suala la baadhi ya wanachama waliotia nia kujipitisha majimboni liliripotiwa huku baadhi ya watu hao wakidaiwa kufanya vikao visivyo rasmi na baadhi ya wajumbe wa mikutano ya majimbo.

**WATEULE WA RAIS**

Miongoni mwa wanachama walojitokeza kutia nia katika ubunge ni waliokuwa wameteuliwa na Rais kushika nyadhifa mbalimbali serikalini kama vile ukuu wa mkoa, ukuu wa wilaya, ukurugenzi wa halmashauri na ukatibu mkuu wa wizara.

Viongozi wakuu wa CCM hao kwa nyakati tofauti walionekana kutokuridhishwa na hatua zao, huku baadhi yao wakiwatahadharisha kuwa wasithubutu kuwania ubunge.

Polepole kwa mfano, alipokuwa katika ziara ya kikazi Kigamboni, alimpiga kijembe mmoja wa wakuu wa mikoa, bila kumtaja jina, kuwa amesikia anawania ubunge katika jimbo hilo. Hata hivyo, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alitia nia na kushika nafasi ya pili katika kura za maoni.

Rais Magufuli, Mwenyekiti wa Taifa wa CCM, aliwaita watu hao wana tamaa na hawatosheki na nafasi walizonazo huku Samia akisema watu hao watakipata wanachostahili huku akitumia msemo wa "mwanakulitafuta, mwanakulipata".

Kuhusu majaliwa ya kupitishwa kwao, Rais Magufuli alisema itategemea atakavyoamka siku hiyo.

Mbali na Makonda, viongozi wengine waliojiengua na kutia nia na nafasi zao kwenye mabano ni Alexander Mnyeti (Mkuu wa Mkoa wa Manyara), Prof. Kitila Mkumbo (Katibu Mkuu Wizara ya Maji), Patrobas Katambi (Mkuu wa Wilaya ya Dodoma)

• ***Imeandikwa na Romana Mallya, Mary Geofrey, Elizabeth Zaya (DAR) na Augusta Njoji, DODOMA.***

# Ofisi nyingine CHADEMA yachomwa moto

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WATU wasiojulikana wamevunja ofisi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Wilaya ya Mbeya Mjini na kuteketeza kwa moto baadhi ya nyaraka muhimu zikiwamo fomu za wagombea ubunge wa viti maalum kupitia chama hicho.

Hilo ni tukio la pili kwa chama hicho ofisi zake kuchomwa moto ndani ya muda wa siku tano. Agosti 13, mwaka huu, ofisi za chama hicho Kanda ya Kaskazini zilizoko jijini Arusha, zilichomwa moto na kuteketeza nyaraka mbalimbali.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Ulrich Matei, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa jeshi hilo linaendelea na uchunguzi ili kuwabaini waliohusika kuchoma ofisi hiyo.

Kamanda Matei alibainisha kuwa uchunguzi wao wa awali umebaini ofisi hiyo haikuwa na mlinzi na ndiyo maana wahusika walitekeleza tukio hilo kwa kuvunja mlango kwanza.

Alisema uchunguzi wa awali pia umebaini kulikuwa na hali ya kutoridhika kwa baadhi wa wanachama wa chama hicho juu ya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya udiwani katika jimbo hilo.

Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Mbeya Mjini, John Mwambigija, aliwaambia waandishi wa habari mjini hapa jana, kuwa alipigiwa simu na katibu wa chama hicho wilaya alfajiri kuhusu kutokea kwa tukio hilo na baada ya taarifa hizo, akakimbia kwenda kwenye ofisi yao akifuatana na wanachama wengine kwenda kuokoa mali.

Alisema walipofika, walikuta baadhi ya nyaraka muhimu za chama na za serikali pamoja na samani za ofisi hiyo zikiwa zimeteketea, hivyo akaliomba Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola kufanya uchunguzi ili kubaini waliohusika na uhuni huo.

Alizitaja nyaraka zingine zilizoteketea kuwa ni pamoja na vitabu vya kanuni za uchaguzi walizokabidhiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa ajili ya wagombea wa nafasi ya ubunge na madiwani.

Mwambigija alidai uchunguzi wao wa awali umebaini lengo la waliotekeleza tukio hilo ilikuwa kuteketeza fomu za wagombea udiwani na za mgombea ubunge wa jimbo hilo, lakini kutokana na moto huo kudhibitiwa kabla haujasababisha madhara makubwa, fomu hizo zilisalimika.

"Ninawaomba wanachama wenzangu wa CHADEMA, tusilipe kisasi kwa mtu yeyote hata kama tunawafahamu waliohusika, pengine walitaka tusiwe na wagombea udiwani na ubunge wa jimbo hili, lakini wameshindwa," alisema Mwambigija.

Alisema chama hicho hakina wasiwasi kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu kwa kuwa kinaamini kitashinda katika jimbo hilo pamoja na kata zote 36 za Jiji la Mbeya.

Kiongozi huyo alisema ofisi hiyo ni nyumba ya mtu na siyo ya CHADEMA na kwamba upande mwingine wa ofisi kuna watu wanaoishi na hivyo waliochoma walikusudia pia kuua watu.

Mtoto wa mmiliki wa nyumba hiyo, Anna Mwansasu, alisema alibaini kuwa ofisi hiyo imechomwa moto usiku wakati amelala baada ya moshi kuingia ndani ya chumba chake.

Alisema alipoona moto ndani ya ofisi hiyo, aliwapigia simu baadhi ya viongozi wa CHADEMA ambao walifika eneo la tukio na kushirikiana na majirani kuuzima moto huo kwa kutumia maji na baadaye walitoa baadhi ya vitu vilivyokuwa vimenusurika.

"Baadhi ya vijana waliokuwa wanaendesha bajaji walikuja tukashirikiana nao kuuzima moto na wakanishauri nizime umeme ili moto usishike nyumba nzima na kweli nilifanya hivyo na sisi huko ndani hatujadhurika," alisema Anna.

Baadhi ya wanachama wa CHADEMA mjini hapa, waliliomba Jeshi la Polisi kudhibiti vitendo vya aina hiyo kwa kuwa vinahatarisha amani ya jiji hilo.

Kissa Swilla, mmoja wa wanachama hao, alisema wanachama wa CHADEMA wakitaka kulipa kisasi kwa matukio ya uchomaji wa ofisi za chama hicho, kuna uwezekano mkubwa wa amani kutoweka na hivyo akaomba waendelee kuwa watulivu.

Tukio la kuchomwa kwa ofisi hiyo ya Mbeya limetokea ikiwa ni siku tano tangu kuchomwa kwa ofisi nyingine ya chama hicho jijini Arusha.

Usiku wa Agosti 13 mwaka huu, ofisi za CHADEMA jijini Arusha zilichomwa na watu wasiojulikana, tukio hilo likithibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi Salum Hamduni.

## HABARI KITAIFA




Ofisi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Jimbo la Mbeya Mjini, ikiwa imefungwa utepe na Jeshi la Polisi kuashiria kuzuiliwa mtu yeyote kuingia ili kupisha uchunguzi kufuatia kubomolewa na baadhi ya nyaraka kuchomwa moto na watu wasiojulikana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# NMB yaipa serikali gawio la bil. 15/-

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

BENKI ya NMB imetoa Sh. bilioni 15. 2 kama gawio kwa serikali ambayo inamiliki asilimia 31.8 ya hisa zote ndani ya benki hiyo.

Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 45 ya gawio lililotolewa mwaka uliopita ambazo serikali ilipata Sh. bilioni 10.48 zilizotokana na faida ya mwaka 2018.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema kuwa, fedha zilizokabidhiwa ni sehemu ya faida iliyopatikana katika mwaka wa fedha 2019 baada ya kuondoa gharama na kodi ambayo ilikiwa Sh. bilioni 45.

Zaipuna alisema mbia mwingine ni Rabo benki ya Uholanzi, ambayo imepata gawio la Sh. bilioni 16. 8 huku Sh. bilioni 13 zikienda kwa wawekezaji wengine zikiwamo taasisi za serikali. Zaipuna alisema kwa mwaka 2019 licha ya benki kuwa chini ya uongozi wa mpito, lakini iliendelea kufanya vizuri na hata kipindi cha mlipuko wa virusi vya corona bado waliendelea kufanya vizuri kwani katika nusu ya mwaka wa fedha 2020 NMB wameshasajili faida ya Sh. bilioni 93.

"Pamoja na hayo, benki inaendelea kufanya vizuri kwa mashirikiano yaliyopo ikiwamo kutoa misaada katika maeneo mbalimbali na kipindi cha majanga ikiwamo Covid-19," alisema Zaipuna.

Kwa mujibu wa mtendaji huyo, benki imeshaanza mkakati wa kuinua kilimo nchini na tayari wamekopesha wakulima Sh. bilioni 800, huku wafanyabiashara wakikopa Sh. trilioni 2.2.

Nyingine ni ununuzi wa madawati 40,000 na kompyuta 1,000 zilizotolewa kwa ajili ya kusaidia shule mbalimbali, na kuwa wameendelea kuwa benki bora kwenye tuzo za jarida la kimataifa la Euro Money kwa miaka minane mfululizo.

Akipokea mfano wa hundi hiyo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema kiwango kilichotolewa ni kizuri sana na kuna matumaini makubwa ya gawio kupanda kwa mwaka huu.

Dk. Mpango aliitaja NMB kuwa miongoni mwa taasisi zinazofanya vizuri zaidi nchini, lakini aliwataka wasibweteke katika siku zijazo bali waongeze ufanisi zaidi katika utendaji kazi wao.

.Hata hivyo, waziri alieleza kusikitishwa na matumizi yasiyofaa katika halmashauri mbalimbali nchini na kumwagiza Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango kuangazia macho yao huko.

Waziri Mpango alirudia kauli yake kuhusu ukubwa wa riba kwamba mikopo inawatenga wenye kipato cha chini, hivyo aliwataka wenye benki kutafuta suluhisho.

Awali Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede, aliahidi kuwa benki hiyo itafanya vizuri zaidi mwaka ujao baada ya kupata Ofisa Mtendaji Mkuu kwani alipokuwa akikaimu hakuwa na nguvu zaidi katika maamuzi.

Dk. Mhede alisema baada ya kumpata mtendaji mkuu, wanaamini benki hiyo itaendelea kuwa imara zaidi na kuwa mfano kwa benki nyingine ndani ya nchi.

# IGP aonya wanasiasa vurugu uchaguzi mkuu

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, amewaonya wanasiasa kuwa vurugu na matusi kwa viongozi wengine haziwezi kumwingiza mtu yeyote madarakani.

Sirro alitoa onyo hilo wakati wa mkutano wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na wadau wa uchaguzi uliohusisha wakuu wa taasisi nyeti za serikali.

Baadhi waliohudhuria mkutano huo ni Kamishna wa Uhamiaji, Anna Makakala, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Brigedia Generali John Mbungo, na Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi.

Wadau wengine waliohudhuria ni viongozi wa vyama vya siasa, Taasisi ya Mwalimu Nyerere na viongozi wa dini.

Katika mkutano huo, IGP Sirro aliwataka wanasiasa kuepuka hasira, akihoji: "Je, Watanzania wakifa utapata faida gani? Kama unataka kufa kwa kupata uongozi, ukifa utamwongoza nani? Kuwahamaisha watu waingie barabarani ni kusababisha machafuko, kama unataka kufa, tumia njia nyingine na siyo ya siasa," alisema.

IGP Sirro alisema Jeshi la Polisi lipo vizuri na litahakikisha amani inaendelea kuwapo Tanzania na kuwataka wanasiasa kuepuka siasa za mihemko na kusababisha vurugu.

Alisema baadhi ya viongozi wa siasa wako tayari kufa wakati wa uchaguzi na kuwakumbusha kuwa wao wataondoka, lakini nchi itabaki.

"Tumejipanga vizuri, kila mnachofanya tunakijua, unayepanga naye usimwamini, tunajua baadhi ya watu wamepanga kujeruhi wengine, wengine wamepanga wachome vituo vya mafuta," alisema.

Kuhusu kulinda kura, aliwakumbusha viongozi wa vyama kuwa sheria haijatamka na kwa kufanya hivyo ni kujiingiza kwenye vitendo vya uhalifu.

IGP Sirro aliitaka NEC ihakikishe inatimiza majukumu yake kwa kuhakikisha vifaa vya uchaguzi, vituo vya kupigia kura na magari ya kubeba kura yanafika kwa wakati ili kutoruhusu vurugu kutokea.

Mwenyekiti wa NEC, Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, alisema ili uchaguzi ufanyike kwa amani na utulivu, viongozi wa vyama vya siasa wanapaswa kuzingatia taratibu zilizowekwa kisheria.

Kamishna Jenerali Idara ya Uhamiaji, Dk. Makakala, alisema uraia ni suala muhimu kisheria na ndiyo msingi imara unaolenga uzalendo, kuitetea, kuilinda na kuipigania nchi kwa namna yoyote.

Msemaji Mkuu wa Idara hiyo na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano, Mrakibu wa Uhamiaji, Paul John Mselle, alitaja baadhi ya mambo yanayoweza kumfanya mtu kupokonywa uraia wake kuwa ni kudanganya, kutokuwa mtiifu wa serikali na kuwa na haki za raia katika nchi nyingine.

Brigedia Generali Mbungo alisema vyama vya siasa vina wajibu wa kulinda sheria ya nchi na kuhakikisha wanachama wao hawajihusishi na vitendo vya rushwa.


Tpb Bank
Grow with us

TPB BANK PLC

TAARIFA KWA WATEJA

Kwa wateja wetu na wadau, kutokana na uamuzi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuunganisha benki ya TIB Corporate na benki ya TPB, tunawaarifu kuwa kuanzia tarehe 28 Agosti 2020 kuanzia saa nne usiku hadi 30 Agosti 2020, matawi yote ya TIB Corporate yatafungwa ili kuruhusu kukamilika kwa shughuli za kuunganisha mifumo ya Tehama. Vilevile huduma za ATMs na Simu za Mkononi hazitapatikana katika kipindi hicho.

Huduma zetu zitarejea tena kuanzia tarehe 31 Agosti 2020 na wateja wote wa TIB Corporate wataweza kupata huduma kutoka katika matawi yao au katika matawi 77 ya Benki ya TPB yaliyopo nchi nzima.

**Ikiwa utahitaji msaada wowote wakati wa uhamishaji wa mifumo, wasiliana na kituo cha huduma kwa wateja cha TPB kupitia nambari za simu 0658/0788-767683 or 0713 162 335**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.***

**Utawala**

215864702

# Lukuvi aunda kamati mpya Kuchunguza mgogoro ardhi

**Na Adam Fungamwango**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameunda timu ya maofisa wa upelelezi toka Jeshi la Polisi kuchunguza mgogoro wa ardhi uliodumu kwa miaka 17 bila ufumbuzi katika Mtaa wa Nyakasangwe, Kata ya Wazo, Wilaya ya Kinondoni.

Lukuvi aliteua timu hiyo jana na kuitambulisha mbele ya wananchi wa mtaa huo alipotembelea na kusema timu hiyo itakuwa na jukumu la kuchunguza wahusika wote kwenye mgogoro huo kwa miezi mitatu mpaka Oktoba, mwaka huu.

Akizungumza mbele ya wananchi hao, alisema amelazimika kuunda timu hiyo kutokana na kutokuridhika na taarifa iliyowasilishwa ofisini kwake na waatalamu wake wa wizarani, ambayo imeonekana kua na dosari nyingi.

Lukuvi aliyeambatana na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, na Mkurugenzi wa Manispaa,

Aaron Kagurumjuli, alisema historia ya mgogoro wa eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 2,878, inaanzia kwenye Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC) lililowahi kuwa na umiliki kwa miaka ya nyuma kabla ya kulirejesha kwa halmashauri.

Mgogoro huo unahusisha makundi mawili ya wananchi wenye umiliki halali wa mashamba kwa kuwa na hati huku wengine wakidaiwa kuwa wavamizi wa maeneo ambao wote kwa ujumla wao ni 3,350.

"Wataalamu wangu wa wizara hawajaleta vielelezo vya kutosha kutoka kwa pande zote zilizohusika kwenye mgogoro huu, hivyo nina mashaka (shaka) na ripoti hii," alisema Waziri.

"Kazi ambayo haijafanyika kwenye kamati hii na ambayo nataka niifanye ni utambuzi wa vielelezo vya umiliki kwa sababu wale watu waliosema wana mashamba historia inaanzia NDC, lakini wataalamu wangu hawakwenda NDC kujua walichukuaje mashamba na ilikuwaje mpaka wakayarejesha," aliongeza.

Waziri aliongeza kuwa makaratasi yaliyofikishwa kwake ni yale yale yaliyoandikwa na Manispaa ya Kinondoni ya wakati huo lakini historia inaonyesha migogoro mingi ya ardhi hutengenezwa na halmashauri, hivyo ni ngumu kupata suluhu kwa mtindo huo kupitia kwenye halmashauri.

Alisema kwenye halmashauri kumekuwapo na tabia ya watu kughushi nyaraka za umiliki wa mashamba na ardhi kwa ajili ya kupoteza ushahidi na kujinufaisha.

"Taarifa za wataalam kuhusu pande zote mbili za mgogoro nadhani si sahihi, na nina mashaka nazo," alisema na kuongeza:

"Nimeamua kuteua wataalamu kutoka Jeshi la Polisi ambalo ndicho chombo chenye mamlaka kwa mujibu wa sheria za nchi kufanya upelelezi huru bila mipaka na kuja na ripoti kamili itakayowezesha kutoa maamuzi (uamuzi) yenye (wenye) haki."

Lukuvi alisema hakuna mwananchi yeyote ambaye atavunjiwa nyumba au kuondolewa kwenye eneo hilo na kwamba serikali itatoa utaratibu wa kuwezesha wale ambao hawana vielelezo vya umiliki wa mashamba kununua maeneo hayo upya ili wapewe hati za umiliki. Kutokana na hali hiyo, aliagiza halmashauri na wananchi kusimamisha kila kitu, ikiwamo ujenzi au uboreshaji wa nyumba, hivyo kila kitu kibaki kama kilivyo mpaka ripoti ya taarifa ya timu aliyoiunda itakapokamilika.



Mafundi wakijenga barabara ya kuelekea kituo cha basi cha Ubungo Mawasiliano jijini Dar es Salaam jana, kwa kiwango cha zege, ambayo kwa muda mrefu imekuwa na mashimo na kusababisha baadhi ya madereva wa daladala kukatisha ruti. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mgombea urais CCK asema makahaba watachapwa viboko 100, jela miezi sita

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA urais kupitia Chama Cha Kijamii (CCK), David Mwaijojele, amesema iwapo wananchi watakipa ridhaa chama chake kushika madaraka, serikali yake itatunga sheria ambayo makahaba, wasagaji na mashoga watakuwa wanachapwa viboko 200 na kwenda jela miezi sita.

Aidha, alisema mafisadi, watakatishaji fedha na wanaotorosha fedha nje watapewa adhabu ya kwenda jela miaka 50 na kupigwa viboko 200 baada ya kuhukumiwa.

Akizungumza katika mahojiano maalum na gazeti hili jana, alisema suala la rushwa limekuwa tatizo sugu nchini, hivyo serikali yake itahakikisha linashughulikiwa ipasavyo ili liishe kabisa.

"Mwili wa mtu si wa kufanyia biashara kingono, makahaba, wasagaji na mashoga wanaitia aibu nchi. Naomba wananchi wanikabidhi nchi nitawanyoosha," alisema Mwaijojele.

Alisema mambo mengine ambayo serikali yake itayapa kipaumbele ni elimu, afya na kuboresha sekta ya kilimo ambayo asilimia kubwa ya Watanzania wanajishughulisha na kilimo kwa ajili ya kuendesha maisha yao.

Mgombea huyo alisema serikali yake pia itahakikisha vyombo vya habari vinakuwa huru zaidi ili kutekeleza majukumu yao vizuri ya kuhabarisha wananchi.

Kuhusu kampeni, alisema chama chake kimejipanga kufika katika mikoa na wilaya zote kwa kutumia fedha ambazo zinachangwa na wanachama na watu wenye mapenzi mema na chama hicho.

"Chama chetu hakina wabunge, hivyo hatupati ruzuku, kwa hiyo fedha za kampeni tutachangisha ndugu jamaa na marafiki, ili kufanikisha kampeni. Nawaomba wananchi waniunge mkono kuchangia chama chetu ili kiingie madarakani na kuwaletea maendeleo ya kweli," alisema.

Alisema maeneo ambayo yeye mgombea urais hatafika kutokana na hali ya uchumi, viongozi wa mikoa, wilaya, tarafa, kata, kijiji na vitongoji watamnadi kwenye mikutano yao ya kampeni.

Pia alisema chama hicho kinacho ilani ambayo kitaitumia kuinadi kwa wananchi ili kukichagua na kushika dola katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

# Kortini tuhuma kupanga ugaidi

**Na Hellen Mwango**

WATU watatu wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakikabiliwa kesi ya uhujumu uchumi yakiwamo mashtaka saba ya kuongoza genge la uhalifu, kupanga mikakati ya ugaidi na kutumia sare za jeshi isivyo halali.

Washtakiwa hao, Halfan Hassan, Adam Kasekwa na Mohamed Lingwenya, walifikishwa mahakamani hapo jana na kusomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba.

Katika kesi hiyo, upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili Serikali Mkuu Shedrack Kimaro, Mawakili wa Serikali Waandamizi Wankyo Simon na Tulimanywa Majigo.

Wankyo alidai kuwa katika shtaka la kwanza la kuongoza genge la uhalifu, washtakiwa wote kati ya Mei Mosi na Agosti Mosi, mwaka huu, katika hoteli ya Aishi, Moshi mkoani Kilimanjaro na katika maeneo mengne ya Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, kwa pamoja na wengine ambao hawakuwapo mahakamani, kwa makusudi walitengeneza mpango wa kutengeneza mikakati ya kigaidi ambayo ni kufanya milipuko katika vituo vya mafuta na mikutano ya hadhara kwa lengo la kuharibu misingi ya kisiasa, katiba, uchumi na sifa ya Tanzania

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa tarehe na maeneo tajwa, washtakiwa hao kwa pamoja na wengine ambao hawakuwepo mahakamani, walishiriki vikao vya mikakati huku wakijua vina muunganiko wa matukio ya ugaidi.

Matukio waliyodaiwa kupanga ni kufanya milipuko katika vituo mbalimbali vya mafuta na mikutano ya madhara kwa lengo la kuharibu misingi ya kisiasa, katiba, uchumi na sifa ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wakili aliendelea kudai kuwa shtaka la tatu linamkabili Kasekwa ambaye anadaiwa Agosti 5, mwaka huu, Katika eneo la Rau Madukani, Moshi, alikutwa na dawa za kulevya aina ya Heroin zenye uzito wa gramu 3.18, shtaka ambalo pia linamkabili mshtakiwa Lingwenya anayedaiwa kukutwa na Heroin zenye uzito wa gramu 1.06.

Katika shtaka la tano, Kasekwa anadaiwa Agosti 5 katika eneo la Rau Madukani, alikutwa na bastola yenye namba A 5340 aina ya Luger bila ya kuwa na kibali cha umiliki na katika shtaka la sita, Kasekwa anadaiwa kukutwa na vilipuzi ambavyo ni risasi tatu bila ya kuwa na leseni ya umiliki

Katika shtaka la saba, Hassan anadaiwa Agosti 10, katika Manispaa ya Temeke jijini Dar es Salaam, kwa lengo la kuhatarisha usalama wa nchi, alitumia sare za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Ilidaiwa kuwa sare hizo zilkuwa suruali ya JKT, suruali nne, fulana moja, koti la mvua, jaketi, kofia tano, maovaroli matano, begi la kubebea vifaa vya lijulikanalo kwa jina la ponjoo, vyeo vinne vya koplo, mikanda minne, soksi pea moja, sweta, beji ya mafunzo ya parachuti, kibuyu cha kunywea maji vyote vikiwa ninmali ya JWTZ pamoja na kisu aina ya AK 47 CCCP.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi. Kimaro alidai upelelezi wa kesi hiyo Bado haujakamilika.

Hakimu Simba alisema kesi hiyo itatajwa Septemba 2, mwaka huu, na washtakiwa walipelekwa mahabusu.

HABARI KITAIFA

# Mwanafunzi mahututi kwa madai kupigwa na mwalimu

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linamshikilia Mwalimu wa Shule ya Msingi Mwendapole, Evata Mboya (50), kwa tuhuma za kumshambulia kwa fimbo mtoto wa miaka 12, mwanafunzi wa darasa la tano wa shule hiyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema tukio hilo lilitokea Agosti 8, mwaka huu, majira ya saa tano asubuhi shuleni hapo.

Alisema siku ya tukio, Mwalimu Mboya alitoa adhabu ya kuwachapa viboko vitatu kila mmoja, wanafunzi 15 akiwamo mwanafunzi huyo, kwa kosa la kupiga kelele darasani.

Alisema, baada ya adhabu hiyo majira ya saa 12, walimu wakiwa ofisini waliingia wanafunzi wakiwa wamembeba mtoto huyo ambaye alikuwa akilalamika maumivu ya kichwa.

Kamanda alisema mtoto huyo alifikishwa katika Hospitali ya Teule ya Rufani ya Mkoa ya Tumbi kutokana na hali yake kutokuwa nzuri na kuhamishiwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili- Mloganzila kwa matibabu zaidi.

"Mtoto anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Mloganzila na mtuhumiwa anaendelea kushikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Pwani. Atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika," alisema Wankyo.

Ofisa Uhusiano wa Hospitali ya Muhimbili tawi la Mloganzila, Neema Mwangomo, alikiri kupokewa kwa mwanafunzi huyo na kwamba kwa sasa yuko kwenye chumba cha uangalizi, madaktari wakipambana kumrejesha katika hali yake ya kawaida.

Mama mzazi wa mtoto huyo, Zakia Mgaya, alisema siku ya tukio alitumwa mtoto kumuita kwa madai kuwa anahitajika shuleni na alipofika alimkuta mwanawe akiwa amelala chini na alipomuita hakuitika.

"Huyu mwalimu anayetuhumiwa kwamba ndiye aliyetoa adhabu kwa mwanangu aliniuliza kama mwanangu ni mtundu nikamwambia hapana, kuna mwalimu mwingine alikuwapo hapo akaniambia mwanangu alidondoka," alisema.

Aliongeza kuwa alitaka kumpeleka mwanawe nyumbani, lakini walimu walimshauri kumpeleka hospitali ya serikali kwa ajili ya matibabu ndipo alipompeleka zahanati ya Mwendapole na kutakiwa kumpeleka kituo cha afya mkoani.

Rehema alisema wakiwa katika kituo cha afya mkoani, walipewa rufani kwenda Hospitali Teule ya Rufani Tumbi kwa matibabu zaidi na hadi kufikia saa 11 jioni ya siku ya tukio mtoto huyo alikua hajazinduka.

"Mwanangu alizinduka Agosti 13 usiku tukiwa katika Hospitali ya Tumbi, lakini hali yake bado ilikuwa haijarejea kama kawaida na tukahamishiwa katika Hospitali ya Mloganzila hadi sasa hali yake haijarejea kuwa sawa," alisema.

Baba wa mtoto, Ally Mikatio, alisema alipewa taarifa na mzazi mwenzake kuwa mtoto ameanguka shuleni na alipouliza walimu wakasema mtoto alikuwa akijisikia vibaya na baadaye kuanguka na wanafunzi wenzake kumpeleka ofisini.

Mzazi huyo alisema, siku ya Alhamisi alipata taarifa kuwa mtoto wake alipata adhabu ya fimbo na si kuanguka kama alivyopata taarifa za awali na kwa sasa mtoto amepata vipimo na kungundulika kuwa damu imevilia kwenye ubongo upande wa kushoto wa kichwa na anatakiwa kufanyiwa upasuaji.



Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe (katikati), akipokea fomu ya kugombea ubunge wa Jimbo la Kigoma Mjini kutoka kwa Msimamizi Msaidizi wa jimbo hilo, Ferdinand Firimbi, mjini Kigoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aishangaa halmashauri kutotoa hati kwa miaka minne

**Na Munir Shemweta, USHETU**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameshangazwa na Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga kushindwa kutoa hati ya ardhi hata moja kwa wananchi katika kipindi cha miaka minne.

Dk. Mabula alionyesha kushangazwa huko jana akiwa katika ziara yake ya kikazi kwenye Halmashauri ya Ushetu baada ya kuelezwa na Mkurugenzi wa Halamshauri hiyo, Michael Matomora, kuwa halmashauri yake haikutoa hati katika kipindi cha miaka minne kutokana na matatizo malimbali ikiwamo upungufu wa watumishi, vifaa vya upimaji na mwitikio mdogo wa umilikishaji ardhi.

Alisema haiwezekani Halmashauri ya Ushetu, aliyoieleza kuwa bado ni mpya, kushindwa kuandaa hati katika kipindi hicho na kumwagiza Kamishna Msaidizi wa Ardhi Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Shinyanga, Ezekiel Kitilya, kupeleka mtaalamu wa ofisi yake kusaidia ukamilishaji wa baadhi ya hati za ardhi zilizoandaliwa.

Taarifa ya ardhi ya halmashauri ya Ushetu iliyotokana na mgawanyo wa iliyokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ambayo ilihamia rasmi makao yake makuu eneo la Nyamilangano mwaka 2016, inabainisha kuwa halmashauri hiyo iliandaa hati 335 lakini ilishindwa kuzitoa kwa wananchi.

Kutokana na maelezo hayo, Naibu Waziri Mabula aliagiza hati hizo kukamilishwa ndani ya mwezi mmoja na kutolewa kwa wahusika.

Dk. Mabula alisema kama kuna shida yoyote ya kitaalamu kuhusiana na uandaaji hati za ardhi, ofisi ya ardhi mkoa wa Shinyanga ipo na inaweza kutoa msaada kwa halmashauri hiyo kurahisisha na kuongeza kasi ya utekelezaji wa suala hilo.

"Mkurugenzi sasa mnakusanya nini katika kodi ya pango la ardhi? Badilisheni utaratibu watu wamilikishwe na kupatiwa hati. Halmashauri yenu bado ni mpya inahitaji mpango kabambe ili watu wasijenge ovyo," alisema.

Dk. Mabula pia alitaka elimu itolewe kwa viongozi wa vijiji vinavyokuwa kwa kasi ili kuwanadaa wananchi wao kupanga vizuri maeneo kwa lengo la kuepuka ujenzi holela ili kuepuka urasimishaji aliouelezea kuwa si wa kudumu. Pia alisisitiza kwamba iwapo viongozi wa halmashauri watashindwa kupanga vizuri miji yao, wategemee kuwa na miji ya ovyo na migogoro ya ardhi .

Mabula pia alitembelea Halmashauri ya Msalala na kuwataka watendaji wa sekta ya ardhi kuongeza kasi ya utoaji hati za ardhi na kuagiza kila mwezi halmashauri hiyo iandae hati 600.

## Mwili uliozuiwa Mloganzila wazikwa

**Na Thobias Mwanakatwe**

HATIMAYE mwili wa Herman Kamwela (65) mkazi wa kijiji cha Isoko, Ileje mkoani Songwe, uliokuwa umezuiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, umechukuliwa na kuzikwa.

Mwili huo ulidaiwa kuzuiwa katika hospitali hiyo kwa siku tano kuanzia Agosti 12, mwaka huu, alipofariki dunia kutokana na kutolipwa kwa gharama za matibabu zilizofikia Sh. 1,581,426.

Gazeti la Nipashe ndilo lilifichua suala hilo na hatimaye likasambaa kwenye mitandao ya kijamii na baadhi ya vyombo vya habari.

Hata hivyo, baada ya malumbano kati ya hospitali hiyo na wananchi wa mtaa wa Machimbo-Segerea ambako marehemu alikuwa akiishi, hatimaye juzi mwili huo uliruhusiwa kuchukuliwa saa 7:00 mchana na kuzikwa saa 10:00 jioni katika makaburi ya Segerea, jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Machimbo, Mariam Machicha, ambaye aliongoza wananchi wa mtaa wake hadi kufanikisha mwili huo kutolewa, akizungumza wakati wa maziko, alizishukuru Hospitali za Muhimbili- Mloganzila, Amana na zahanati ya Segerea kwa jitihada za kuokoa maisha ya Kamwela.

Machicha alivishukru vyombo vya habari, hususani gazeti la Nipashe, kwa kuibua sakata hilo na hatimaye kufanikisha kuuchukua mwili huo hospitalini. Pia aliwashukru wananchi wa mtaa huo kwa ushirikiano walioutoa wakati wa tukio hilo.

Gaseti hili juzi liliripoti habari za tukio hilo na Machicha alisema mwananchi huyo ambaye hana ndugu jijini Dar es salaam, alifariki dunia Agosti 12 na hadi Jumatatu mwili wake ulikuwa haujachukuliwa.

Alisema Kamwela ambaye alikuwa akisumbuliwa na magonjwa mbalimbali, mara ya kwanza alipelekwa katika zahanati ya Segerea baadaye Hospitali ya Amana na Julai 26, mwaka huu, alihamishiwa Mloganzila alikokuwa akipatiwa matibabu hadi mauti yanamkuta.

"Kamwele alikuwa mkazi wa mtaa wangu na alikuwa hana ndugu yeyote hapa alipofariki wananchi wa mtaa huu nikiwemo mimi (mwenyekiti) tulikwenda Mloganzila kwa lengo la kuchukua mwili ili tukazike lakini tukaambiwa na uongozi wa hospitali hatuwezi kuuchukua hadi tulipe Sh. 1,581,426, tukashindwa, "alisema Machicha.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila upande uwajibike kufanikisha uchaguzi

WAKATI huu wa kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, changamoto kadhaa zimeanza kuonekana, yakiwamo malalamiko kutoka kwa vyama vya siasa na wagombea.

Yapo malalamiko ambayo yamewasilishwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na mengine hayajawasilishwa kwa mamlaka yoyote, lakini ni dhahiri kuwa yapo malalamiko hata kama yamethibitika kuwa kweli ama la.

Kwa mfano, kuna vyama vinadai kuwa wagombea wao wamenyimwa fomu za kugombea ubunge na udiwani katika maeneo kadhaa, na kuelekezwa na wasimamizi wa uchaguzi kuwa sababu za kunyimwa ni kutokana na kuwa wagombea kadhaa kutoka vyama hivyo walishazichukua.

Kuna madai mengine yenye tuhuma nzito yanayotolewa na wanasiasa, lakini hatuwezi kuyazungumzia hapa kutokana na kukosa ushahidi.

Hata hivyo, madai kuwa baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi wanawanyima fomu wagombea halali wa vyama hayanabudi kuwasilishwa NEC na chombo hicho kuyashughulikia na kutoa mrejesho kwa umma.

Tunasema na kusisitiza hivyo kwa kuwa haiwezekani mtu binafsi ambaye si mteuliwa wa chama cha siasa akaenda Tume na kupewa fomu bila msimamizi kuthibitisha bila kuacha shaka yoyote kuwa ndiye aliyeteuliwa na chama husika.

Wateuliwa wote wa vyama vya siasa wanajulikana, na vyama vyao vinapaswa kuulizwa pale inapotokea mtu asiyehusika kwenda NEC na kudanganya kuwa ni mgombea wa chama fulani.

Tunaona kwamba kama kuna matukio ya namna hii, ni vizuri wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo kuketi na vyama kuweka sawa mambo ili kujiepusha na malalamiko na matukio mengine yanayoweza kuharibu uchaguzi huo na kuufanya usiwe huru na haki.

Suala la kuufanya uchaguzi huo kuwa wa amani, utulivu na huru na haki ndilo tegemeo la kila Mtanzania na Jumuiya ya Kimataifa. Rais John Magufuli amekuwa akilizungumza na kulisisitiza hilo mara kwa mara.

Kadhalika, viongozi wa dini wamekuwa na wanaendelea kusisitiza amani na utulivu kutawala katika kampeni hadi kwenye uchaguzi wenyewe, hivyo kamwe mtu yeyote asiruhusiwe kwa namna yoyote awe chanzo cha kuharibu uchaguzi wetu.

Ndio maana wasimamizi na wasaidizi wao wanatakiwa kuisoma na kuielewa sheria ya uchaguzi na kanuni zake, miongozo pamoja na maelekezo yanayotolewa na NEC.

Jambo muhimu na la kusisitiza ni kuwa wadau wote wa uchaguzi wahakikishe kuwa malalamiko yote yanawasilishwa na kushughulikiwa na vyombo ambavyo vimewekwa kisheria na kikanuni.

Katika kusisitiza hilo, NEC imesema changamoto zinazojitokeza katika uchaguzi ni watu kuingia wakiwa na sheria na kanuni zao bila kuheshimu zilizowekwa na nchi.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji mstaafu, Semistocles Kaijage, akizungumza katika kikao cha NEC na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam juzi, alisema changamoto hizo zinasababishwa na vyama vya siasa na watu kutokuwa na utayari wa kufuata na kutekeleza sheria za nchi. Alisema hakuna uchaguzi katika nchi yoyote unaofanyika bila kufuata katiba, sheria, maelekezo na maadili.


Alisema kasoro zilizojitokeza katika uchaguzi kadhaa ukiwamo mdogo huko nyuma ni kwa sababu malalamiko hayakupelekwa kwenye Mamlaka ya Kamati za Maadili ya Uchaguzi.

Akinukuu kifungu cha 5.11 katika kitabu cha Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani cha mwaka 2020, chini ya kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura ya 343, kinachozungumzia Mamlaka ya Kamati za Maadili ya Uchaguzi ngazi ya kitaifa, jimbo na kata katika kutoa adhabu, alisema kamati hizo zinaweza kuchukua hatua kwa kuagiza upande uliokiuka maadili kusahihisha kosa au makosa yaliyotendeka na iwapo italazimu, kuuomba umma msamaha na kutoa onyo au karipio kwa maandishi.

Tunasisitiza kuwa uwajibikaji wa kila mmoja na kutenda haki ndiyo siri ya kufanikisha uchaguzi mkuu wa Oktoba, na kuwaacha Watanzania wakiwa wamoja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tukumbuke kujisaidia ovyo si salama kiafya, tubadilike

Na Sabato Kasika

KWA hali ilivyo sasa, ni wazi kwamba kuna haja ya kuwapo elimu ya kutosha kwa baadhi ya watu, ili wabadilike na kuachana na mtindo wa kuchafua mazingira hali ambayo inaweza kuhatarisha afya zao na za wengine.

Imekuwa ni kama jambo la kawaida kukuta baadhi ya vituo vya daladala, jijini Dar es Salaam vikiwa na harufu kali ya haja ndogo hali inayoashiria kwamba, wapo baadhi ya watu wanaojisaidia ovyo katika vituo hivyo.

Ni mambo yanayofanyika kukiwapo kampeni na elimu ya kila namna kutoka kwa jamii ikitakiwa kuachana na tabia hiyo, isiyofaa kwa maisha binadamu.

Najua huko tulikotoka hali ilikuwa mbaya zaidi, ingawa na leo tuliko si pazuri zaidi, kwa maana yana asilimia ya kujikomboa kififikra na kitiba.

Mazingira ya aina hiyo si salama kiafya, hivyo hatua stahiki zinatakiwa kuchukuliwa ikiwamo kuwaelimisha wahusika na hata ikibidi, kuwachukuliwa hatua za kisheria, ili kukomesha tabia hiyo.

Inawezakana si ajabu kukuta kwenye kituo cha daladala kuna choo, lakini baadhi ya watu hawaendi katika kujisaidia humo, badala yake wanakwepa na kujisaidia mitaroni, hali inayosababisha kuwapo harufu kali ambayo ni hatari kiafya.

Hivi kweli mtu anashindwa kulipia shilingi 200 au 500 ya kulipia huduma ya choo, au ni mazoea ya uchafuzi wa mazingira? Kuna haja ya mamlaka husika kuchukua hatua kulinda afya za wengine.

Kwa mfano ni katika kituo kikuu cha daladala Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam, kuna vituo viwili vya daladala na kuna huduma za choo cha kulipia, lakini ajabu ni kwamba, baadhi ya watu hawaendi kupata huduma hiyo.

Ninasema hivyo, kwa sababu kuwapo kwa harufu kali ya haja ndogo kwenye moja ya vituo hivyo, ni wazi kuna watu hujisaidia ama kwenye mitaro au kujificha nyuma ya magari kumaliza haja zao huko.

**Ni mambo yanayofanyika kukiwapo kampeni na elimu ya kila namna kutoka kwa jamii ikitakiwa kuachana na tabia hiyo, isiyofaa kwa maisha binadamu.**

Wakati baadhi ya watu wakijisaidia haja ndogo ovyo, wale wanaofanya biashara ndogo ikiwamo uuzaji wa vyakula kama ugali, wali, chipsi, vitumbua, maandazi, mihogo ya kukaanga na matunda nao ni muhimu wasaidie.

Hii inatokana na ukweli kwamba, baadhi yao wanafanyia biashara katika maeneo ambayo si safi na wapo pia wanaochafua mazingira ya biashara, hali ambayo ni hatari kwa afya zao na wateja wao.

Kimsingi, muungwana sina tatizo na shughuli zao za kiuchumi, ila kuna haja ya kukumbushana jambo moja la muhimu ambalo wahusika kuzingatia, usafi, huku msingi mkubwa ukiwa ni kulinda afya.

Isichukuliwe kama jambo la kawaida mtu kuzoea.

HABARI KITAIFA

# TAKUKURU yarejesha mamilioni ya mstaafu

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, (TAKUKURU) mkoani Shinyanga, imeokoa Sh. milioni 20 za mtumishi mstaafu wa Idara ya Afya, Alex Gabagu zilizokuwa zimechukuliwa na kampuni ya ukopeshaji ya Nyakiha.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga, Hussen Mussa, aliwaambia waandishi wa habari jana mjini hapa kuwa, mstaafu huyo alikopeshwa na kampuni hiyo Sh. miloni sita kwa makubaliano ya kurejesha Sh. milioni 26 baada ya kupata mafao ya kustaafu.

Alibainisha kuwa, baada ya mstaafu huyo kupata mafao yake, alipeleka deni lake kwenye kampuni hiyo ya Nyakiha kiasi cha fedha Sh. milioni 26, mkopo ambao TAKUKURU iliuona ni dhuluma na kutokana ma wakopeshaji kujipatia faida ya milioni 20, hivyo kuamua kuzirejesha fedha hizo kwa mstaafu huyo.

"TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga baada ya kuletewa malalamiko na mstaafu huyu juu ya kudhulumiwa fedha zake na Kampuni ya Nyakiha kwa mkopo huo unaoumiza, tukaingia kazini na tumefanikiwa kuokoa fedha zake zote na tumemkabidhi," alisema Mussa.

Alisema taasisi hiyo pia imefanikiwa kumpatia stahiki zake mfanyakazi Yasini Suleimani wa kampuni binafsi ya Hasmukh Morarji, inayojishughulisha na uuzaji wa vocha na miamala, ambaye aliachishwa kazi kinyume cha taratibu na kunyimwa haki zake zote ikiwa ni pamoja na mshahara wa miezi miwili.

"Mtumishi huyo aliachishwa kazi mwaka 2018 na baada ya kuona hapati haki yake, mwaka huu akatoa taarifa kwetu (TAKUKURU). Baada ya kufanya ufuatiliaji wa kina tukabaini mtumishi huyo alionewa na kufanikisha kumpatia stahiki zake zote Sh. 7,203,700. (milioni 7.203).

Wawili hao walionufaika na utendaji wa TAKUKURU, kwa nyakati tofauti jana, waliishukuru taasisi hiyo kwa kupigania haki za wanyonge huku wakitoa wito kwa wananchi wengine waliodhulumiwa kufika kwenye taasisi hiyo ili wapate msaada.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Angellah Kairuki (kulia), akimsikiliza kwa makini Meneja wa Kiwanda cha Konyagi (TDL), Aranyaeli Ayo (kushoto), alipofanya ziara ya kikazi katika kiwanda hicho, Chang'ombe jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni Mkurugenzi wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Maduhu Isack Kazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi wahamasika kuchangia damu

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

UPUNGUFU wa damu wa muda mrefu uliokuwa ukiikabili Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, umepungua baada ya wananchi mbalimbali kuhamasika na kujitokeza kuchangia.

Mratibu wa Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS) Mkoa wa Morogoro, Hashim Ally, alisema juzi kuwa kumekuwa na ongezeko la watu wanaochangia damu, hivyo kufanya uniti 300 kukusanywa kila mwezi tofauti na ilivyokuwa awali.

"Kipindi cha nyuma kulikuwa na uhaba mkubwa wa damu katika hospitali hii na mkoa mzima kwa ujumla kwani kwa mwezi tulikuwa tunakusanya uniti 100 pekee, lakini kwa sasa kuna ongezeko kubwa la uchangiaji wa damu," alisema Ally.

Kwa muda mrefu, alisema katika mkoa kulikuwa na uhaba mkubwa wa damu na hiyo ilisababishwa na mlipuko wa ugonjwa hatari wa corona, lakini baada ya ugonjwa huo kupungua, wananchi wengi wamehamasika.

Ally alisema mahitaji ya damu salama mkoani hapa ni mengi kutokana na ajali nyingi za barabarani ambazo zimekuwa zikitokea kila siku, hivyo kitendo cha kutokuwa na damu salama ya kutosha, husababisha wagonjwa kupoteza maisha.

Mratibu huyo aliwataka wananchi kuendelea kujitokeza ili kuchangia damu kwa kuwa mbali na kwamba kwa sasa tatizo hilo limepungua, bado kuna uhitaji mkubwa wa damu katika hospitali hiyo kwa ujumla.

Katika hatua nyingine, TRCS imetoa vifaa kinga dhidi ya magonjwa ya mlipuko katika vituo vya kulelea watu wenye mahitaji maalumu kwa Wilaya za Ulanga, Kilombero na Morogoro vyenye thamani ya Sh. milioni 30.

Kibwana Mlekwa, Mwenyekiti wa TRCS Mkoa wa Morogoro alisema chama chake kimeamua kutoa vifaa kinga hiyo kwa lengo la kuwa karibu na jamii inayowazunguka hususani kwa wale wenye uhitaji.

Mlekwa alisema kitendo cha kuwa karibu na jamii kutawahamasisha wananchi mbalimbali kujitokeza kuchangia damu hali inakayofanya mkoa kuwa na akiba ya kutosha ya damu salama.

## Vijana 105 wapata ajira kiwanda cha pamba

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

VIJANA 105 wilayani hapa wamepata ajira katika kiwanda cha kuchakata pamba kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahama (KACU).

Kutokana na kufunguliwa kwa kiwanda hicho, baadhi ya wananchi wamesema kimesaidia kupunguza wimbi la ukosefu wa ajira kwa vijana wanaozunguka kiwanda hicho licha ya kuwa na ajira za muda.

Wananchi hao wamesema kiwanda hicho kabla ya kusitisha shughuli za uzalishaji awali, kilikuwa kimeajiri vijana wengi kutoka Halmashauri za Msalala, Ushetu na Mji Kahama na baada ya kufungwa vijana wengi walikosa ajira na asilimia kubwa waliingia kwenye uhalifu.

Kauli hiyo waliitoa juzi wakati wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti kiwandani hapo walipofika kuangalia uchakataji wa pamba unavyoendelea na uongozi wa kiwanda hicho walivyojipanga kutatua ukosefu wa masoko kwa wakulima kwa kununua pamba kwa bei nzuri.

Suzan Samuel, mmoja wa wafanyakazi wa kiwanda hicho, ujio wa kiwanda hicho umesaidia kupunguza wimbi la vijana mitaani wasio na kazi kwa kuwapatia ajira za muda na kusababisha kutokuwapo kwa vitendo vya uhalifu.

Naye Samson Andrew alisema kufunguliwa kwa kiwanda kumesababisha kupunguza malalamiko baina ya wakulima na kampuni za ununuzi wa zao hilo kwa kununua pamba kilo moja kwa Sh. 900, hivyo kufanya wananchi kuhamasika kuzalisha pamba kwa wingi msimu ujao.

Mhandisi wa Kiwanda hicho, Hemerius Magege, alisema wameajiri vijana 105 wanaozunguka kiwanda, 10 wakiwa mafundi na 95 wakiwa wabebaji wa magunia ya pamba kutoka kwenye magari na kupeleka kwenye maghala na uchambuzi wa pamba.

Alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kuchakata marobota 140 kwa siku na baada ya kuzindua kwa kiwanda watakuwa na uwezo wa kuzalisha marobota 200.

Hata hivyo, Mhandisi Magege alisema kiwanda kinakabiliwa na uhaba wa vifungashio ambavyo vilichelewa kufika kutokana na janga la corona.

# Mwanafunzi la tano apewa ujauzito

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

JESHI la Polisi mkoani Shinyaga linamshikilia Paschal Coloneli (27), kwa tuhuma za kumpa ujauzito mwanafunzi wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Ibadakuli, Manispaa ya Shinyanga (15) na kukatisha masomo yake.

Ofisa Elimu Sayansikimu na Afya wa Shule za Msingi Manispaa ya Shinyanga, Beatrice Mbonea, alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha Shirika la (YWCA) la mkoani Shinyanga, linalojishughulisha na utetezi wa haki za watoto, vijana na wanawake lilipotambulisha mradi wa kijamii kwa ajili ya watoto na familia utakaotekelezwa Kata ya Ibadakuli.

Alisema tatizo la wanafunzi kuendelea kupewa ujauzito katika manispaa hiyo bado ni kubwa ikiwamo kata hiyo, akibainisha kuwa mwezi uliopita, mwanafunzi huyo alikatisha masomo yake baada ya kubainika ana ujauzito.

"Kwenye mradi wenu huu mnapokuwa mkitoa elimu ya afya ya uzazi kwa wasichana kwa ajili ya kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, elimu hiyo inapaswa pia kutolewa na kwa wanaume ambao ndiyo watiamimba, ili vitendo hivi viishe, vimekuwa vikizima ndoto za wanafunzi wa kike," alisema Mbonea.

Mkurugenzi wa Shirika la Agape, John Myola, linalojihusisha na utetezi wa haki za watoto mkoani Shinyanga, alilaani vitendo vya wanafunzi kuendelea kupewa ujauzito na kukemea tabia ya wazazi na viongozi kupewa vitu vidogo na watuhumiwa na kumaliza kesi hizo kimyakimya.

Ofisa Miradi wa YWCA, John Eddy, akizungumza wakati wa kutambulisha mradi wao mpya, alisema umejikita katika utoaji wa elimu ya afya ya uzazi, lishe, usafi pamoja na uhakika wa kipato, walengwa wakubwa wakiwa ni watoto na wasichana wenye ujauzito.

Alisema katika utoaji wa elimu hiyo, watoto watafundishwa namna ya kuwa safi ili kuepukana na magonjwa ya mlipuko, wasichana wenye ujauzito watapewa elimu ya matunzo bora ya mtoto likiwamo suala la lishe na elimu ya ujasiriamali ili wajikwamue kiuchumi na kulea familia zao.

Alisema mradi huo utakuwa wa miezi 12 na utakamilika Juni mwakani baada ya utekelezaji wake wa awali kuanza Julai mwaka huu, na utagharimu Sh. milioni 18.468 zinazotolewa kwa ufadhili wa Shirika la Firelihgt la Marekani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Debora Magiligimba, alithibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo na kusema kuwa leo ataeleza hatua zinazochukuliwa na jeshi hilo baada ya uchunguzi wake.




Wadau wa zao la korosho (hawako pichani), wakipewa maelezo na Meneja wa Benki ya Exim tawi la Mtwara, Ramadhani Magera, kuhusu huduma za kilimo zinazotolewa na benki hiyo, wakati wa mkutano mkuu wa wadau hao, uliofanyika mkoani Lindi, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni yachangia matangi ya maji shule za umma Dar

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuadhimisha miaka 100 ya utoaji huduma kwenye soko la bima, Kampuni ya UAP Insurance Tanzania imetoa msaada wa matangi 40 ya kuoshea mikono kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi msaada huo, Mkurugenzi Mtendaji wa UAP, Stephen Lokonyo, alisema mchango huo ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya uwajibikaji kwa jamii na umelenga kuhakikisha wanafunzi wanakuwa kwenye mazingira salama wakati wote wawapo shuleni na kupunguza hatari ya kupata magonjwa.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi na kwamba matangi hayo yatasaidia kuhakikisha wanafunzi wananawa mikono yao kwa maji safi na sabuni, hivyo kuhakikisha mazingira salama kwa watoto shuleni.

Kampuni hiyo ni kampuni tanzu ya kampuni ya UAP Holdings PLC inayotimiza miaka 100 tangu kuanzishwa mwaka 1920.

"Tunafarijika kuunga mkono jitihada za serikali na wadau wengine katika kuhakikisha kwamba wanafunzi ambao ni taifa la kesho wanapata elimu bora. Msaada huu utahakikisha kwamba wanafunzi wanapata elimu katika mazingira ambayo ni salama kwa afya zao muda wote," alisema.

Matangi hayo yatasambazwa kwenye shule za msingi na sekondari za mkoa wa Dar es Salaam kulingana na mahitaji kama itakavyoelekezwa na Ofisi ya Elimu Mkoa.

Akipokea msaada huo, Ofisa Elimu Taaluma Mkoa wa Dar es Salaam, Boniphace Wilson, alipongeza hatua hiyo akisema kwamba itasaidia kuongeza kasi ya udhibiti wa milipuko ya magonjwa shuleni na kufanya mazingira ya kujifunzia kuwa salama zaidi.

"Tunawapongeza UAP Tanzania kwa kuona umuhimu wa kutoa matangi haya kwa ajili ya shule zetu za Mkoa wa Dar es Salaam, hii itasaidia kuhakikisha wanafunzi wanapata nafasi ya kuosha mikono yao kwa maji safi na sabuni na kuleta usalama wa mazingira ya kujifunzia," alisema.

Alisema msaada huo ni utekelezaji wa sera ya uwajibikaji kwa jamii ambayo UAP imekuwa ikiendesha katika maeneo mbalimbali ikiwamo afya, elimu pamoja na mazingira tangu ilipoanza kutoa huduma hapa Tanzania.

## Wanawake waongezeka huduma afya ya uzazi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ametaja mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka mitano ikiwamo kuongezeka kwa wanawake wanaotumia huduma za afya ya uzazi kabla ya ujauzito na baada ya kujifungua.

Amesema idadi yao imeongezeka kutoka asilimia 32 mwaka 2015/19 hadi asilimia 43 mwaka 2019/20.

Ummy alibainisha takwimu hizo jana jijini hapa alipotoa taarifa ya afya ya uzazi na mtoto nchini kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2019/20.

Alisema kwa kipindi hicho, Tanzania imeendelea kupiga hatua katika utoaji wa huduma za afya hususan afya ya uzazi na mtoto ambapo hatua hizo ni pamoja na kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma.

Waziri huyo alisema vituo vya huduma za upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni vimeongezeka kutoka 192 hadi 586, sawa na ongozeko la vituo 394.

"Pia, ongezeko la bajeti ya dawa katika Wizara ya Afya limeimarisha hali ya upatikanaji wa dawa muhimu kwa ajili ya afya ya uzazi na mtoto kutoka asilimia 53 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 96 Juni mwaka 2020," alisema.

Alibainisha kuwa uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali kwenye miundombinu ya utoaji wa huduma za afya, umeongeza idadi ya vituo vya huduma kwa ajili ya watoto wachanga wanaozaliwa wakiwa na shida ya kupumua, uzito pungufu na maambukizi ya bakteria kutoka vituo 14 mwaka 2015 hadi vituo 104 mwaka 2020, sawa na ongezeko la vituo 90.

Ummy alisema vituo vinavyotoa huduma ya kangaroo ikiwa ni njia ya kiasili ya kumtunza mtoto aliyezaliwa njiti, pia vimeongezeka kutoka 80 mwaka 2015 hadi kufikia 104 mwaka 2020.

"Katika kipindi cha miaka mitano Serikali imefanya upanuzi wa Hospitali 3 za rufaa za Kanda,Hospitali ya Mtwara,Burigi ambayo ni ujenzi mpya na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambapo jengo kubwa la ghorofa tano lenye uwezo wa vitanda 223 maalum kwa ajili za huduma za mama na mtoto," alisema.

Alisema kwa kipindi hicho, serikali pia imeongeza vituo vya upimaji wa saratani ya mlango wa kizazi kutoka vituo 176 mwaka 2015 hadi kufikia 650 mwaka huu.

Waziri Ummy alisema upatikanaji wa damu salama kwa ajili ya kina mama na watoto, pia umeongezeka kutoka chupa 196,735 mwaka 2015 hadi chupa 309,396 mwaka huu, sawa na ongezeko la asilimia 57.

HABARI KITAIFA

# Mwalimu jela miaka 30 kwa kubaka mwanafunzi

**Na Mwandishi Wetu**

MWALIMU George Ngaru (32) aliyepangiwa kuhudumu Shule ya Sekondari Mahiwa Kata ya Nyangao, Wilaya na Mkoa wa Lindi, amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani, baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mwanafunzi wake (jina limehifadhiwa).

Mbali na adhabu ya kifungo, mahakama hiyo imeamuru mshtakiwa atakapomaliza adhabu yake kumlipa mlalamikaji anayesoma kidato cha tano fidia ya Sh. milioni 2.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mkoa wa Lindi, Elimo Massawe, baada ya kuridhishwa pasipo shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

**Mbali na adhabu ya kifungo, mahakama hiyo imeamuru mshtakiwa atakapomaliza adhabu yake kumlipa mlalamikaji anayesoma kidato cha tano fidia ya Sh. milioni 2.**

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Hakimu Massawe alimpa mshtakiwa nafasi ya kujitetea, ambapo aliiambia Mahakama imwonee huruma kwa madai ni yatima, mkosaji wa mara ya kwanza na anayo familia inayomtegemea, hivyo kama atapewa adhabu kali kutaifanya ikose huduma zake.

Baada ya utetezi huo, Mwanasheria wa Serikali, Emmanuel John, aliiomba mahakama impe mshtakiwa adhabu kali, ili liwe fundisho kwake na wengine wenye tabia za kushiriki mapenzi na wanafunzi.

Hakimu Masawe akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 04/2020, kupitia vifungu vya (130) kifungu kidogo (1) na kifungu cha 3 (C) pamoja na 131, alisema amesikia maombi ya pande zote mbili, lakini sheria imemfunga mikono na kumhukumu kifungo cha miaka 30 jela na kumlipa mlalamikaji fidia ya Sh. 2,000,000.

Awali ilidaiwa na John kuwa Februari Mosi mwaka huu, majira ya alasiri, Ngalu alimtuma mwanafunzi wa kiume amuitie mwanafunzi huyo nyumbani kwake, na hakuweza kurejea mapema, hivyo kumshtua mlinzi wa shule husika na kutoa taarifa kwa mkuu wa shule.

John aliiambia Mahakama baada ya mwanafunzi huyo kuchelewa kutoka ndani, Mkuu wa Sekondari Mahiwa aliwaita walimu wenzake kumfuatilia na kufanikiwa kumkuta akiwa chumbani na mwalimu huyo, kisha walimchukua na kumpeleka hospitali kufanyiwa uchunguzi na kubainika kuwa alifanya ngono na mwalimu huyo.



Wananchi wakivuka sehemu ambayo hairuhusiwi, licha ya kuwapo kwa daraja la juu la waenda kwa miguu katika barabara ya Morogoro, eneo la kituo cha mabasi ya mikoani cha Ubungo stedi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TAWIRI yataja sababu ulaji wanyamapori

**Na Salome Kitomari**

TAASISI ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), imesema sababu za kuongezeka kwa ujangili wa kitoweo cha wanyamapori kwa ajili ya protini itokanayo na wanyama pamoja na ongezeko la idadi ya watu.

Akiwasilisha mada kwenye warsha ya waandishi wa habari za uhifadhi na utalii iliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET) na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Mwakilishi wa TAWIRI, Iddi Lipende, alisema utafiti uliofanyika umebaini ndiyo sababu kuu kwa maeneo ya vijijini.

Aliwasilisha mada kuhusu uhusiano wa wanyamapori, masoko na kusambaa kwa magonjwa yatokanayo kwa wanyama.

Alisema walibaini kuwa nyamapori imekuwa ni kichocheo cha jamii ya vijijini kula nyama hiyo kwa ajili ya kupata protini iliyopo kwao.

Alisema watu wa mjini hupendelea nyama hizo kama utamaduni, ladha na ufahari.

"Kwa sasa kuna mabadiliko sana kwenye uwindaji haramu, wanatumia teknolojia za kisasa tofauti na matumizi ya mishale, huku maboresho ya miundombinu kwenye misitu na usafiri kwenda maeneo mbalimbali yamekuwa kichocheo," alisema.

Alisema magonjwa ya wanyama kwenda kwa binadamu ni mara chache, lakini yakitokea ni rahisi sana kusambaa kwa kasi kwa binadamu, huku akitoa mfano wa ugonjwa wa ebola, kimeta na kichaa cha mbwa.

Alisema ipo haja kwa jamii kutambua kuwa wanyamapori hawataki usumbufu na kuingiliwa maeneo yao na ni vyema wakachukua hatua za kutoingia kwenye maeneo hayo.

Alisema yapo magonjwa ambayo husambaa kwa kasi kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu ambayo tiba yake ni ngumu sana na ndiyo maana kumekuwa na msisitizo wa kuhakikisha hakuna mwingiliano baina ya pande hizo.

Alisema ugonjwa wa kichaa cha mbwa husambaa kwa kasi na wakati mwingine kuingia kwa binadamu, na mbwa ni wale walioingia hifadhini wakiwa na wachungaji wa mifugo ambao huingiza mifugo maeneo yaliyohifadhiwa.

Aidha, alisema ugonjwa wa corona chanzo chake ni kutoka kwa mnyama kuja kwa binadamu.

# Wazee wataka kupatiwa vitambulisho huduma afya

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

BARAZA la Wazee mkoa wa Morogoro limetakiwa kuhakikisha linasaidia kupatikana kwa vitambulisho vya utambuzi kwa wazee zaidi ya 50,000 ili waweze kufikiwa kirahisi na huduma za kijamii ikiwamo huduma za afya.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kusilya Ukio, wakati akizindua Baraza la Wazee wa mkoa huo baada ya kukamilika uchaguzi wa viongozi wapya.

Alisema kati ya wazee 78,601, waliopo mkoani hapa, ni wazee 44,000 ambao wanafikiwa na huduma za afya.

"Vitambulisho vya utambuzi ni muhimu sana, hakikisheni wazee wote waliobaki wanavipata ili viwasaidie kupata huduma za afya pamoja na kwamba huduma ni bure, lakini kwa sasa tunafikiria wazee wajiunge na CHF iliyoboreshwa, ambayo ipo hadi vijijini...itawasaidia kupanua wigo wa kupata huduma." alisema Dk. Ukio.

Awali akitangaza matokeo ya viongozi wapya waliochaguliwa, msimamizi wa uchaguzi huo, Dk. Bwakisha John, alisema kuwa aliyechaguliwa nafasi ya mwenyekiti wa baraza hilo mkoa ni Samuel Mpeka, huku msaidizi wake akichaguliwa Leah Mtemizali.

Alisema pamoja na mambo mengine, viongozi hao wanapaswa kujikita katika kushughulikia changamoto zinazowakabili wazee wenzao kwa kuzifikisha ngazi husika ili ziweze kufanyiwa kazi.

"Niwakumbushe tu wazee wangu kwamba jukumu mlilonalo ni kubwa hasa katika kupigania masilahi ya wazee wote wa mkoa wa Morogoro kwa kuingia katika vikao muhimu vya maamuzi mbalimbali ili kutoa ushauri wenu," alisema Dk. Bwakisha.

Kwa upande wao viongozi waliochaguliwa walisema miongoni mwa chanagamoto ambazo zinawakabili wazee wengi hasa waliostaafu ni pamoja na kutokuwapo kwa sheria ya kupatiwa pensheni.

Leah Mtemizali, makamu mwenyekiti wa baraza hilo, alisema kwa sasa wastaafu nchini hawana pensheni za kustaafu kama ilivyo kwa mataifa mengine, jambo linalowafanya wazee wengi kujikuta wakiishi katika maisha magumu.

**Niwakumbushe tu wazee wangu kwamba jukumu mlilonalo ni kubwa hasa katika kupigania masilahi ya wazee wote wa mkoa wa Morogoro kwa kuingia katika vikao muhimu vya maamuzi mbalimbali ili kutoa ushauri wenu.**

# Taasisi za fedha zatakiwa kupunguzia wananchi riba

Na Enock Charles

TAASISI za kifedha nchini zimetakiwa kuwa msaada kwa wananchi kwa kutoa riba nafuu zinazoweza kuwasaidia wananchi kiuchumi kuliko kutaka faida kubwa inayoweza kusababisha maumivu kwa wananchi wa hali ya chini.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa benki ya NCBA jijini Dar es Salaam jana, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, amesema serikali haitavumilia taasisi za kifedha zenye malengo ya kuwakandamiza wananchi na kudidimiza uchumi wao na uchumi wa Taifa kwa ujumla.

**Nasisitiza ya kuwa juhudi zetu zitakuwa za kidijitali, Benki ya NCBA itawaweka watu na wateja wetu katikati ya uvumbuzi.**

"Sote tumekuwa mashahidi tukisikia baadhi ya taasisi za kifedha zimekuwa na masharti yasiyokuwa rafiki kwa Watanzania wetu na benki zimekuwa na masharti magumu ya mikopo kwa wananchi wakiwamo vijana wetu na kinamama kufika na kuhudumiwa kwa urafiki," alisema Dk. Kijaji.

Dk. Kijaji pia alizitaka taasisi za kifedha kuwafikiria wakulima wadogo katika suala la mikopo kwa masharti nafuu ili kuharakisha ukuaji wa kilimo nchini ambacho ndio tegemeo la wananchi walio wengi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Benki hiyo, Margaret Karume, alisema mojawapo ya malengo ya benki hiyo ni kuchochea mafanikio ya wanaojituma, hivyo kuongeza ukuaji wa uchumi wa Taifa huku njia za kidijitali zikipewa kipaumbele katika huduma mbalimbali za benki hiyo.

"Nasisitiza ya kuwa juhudi zetu zitakuwa za kidijitali, Benki ya NCBA itawaweka watu na wateja wetu katikati ya uvumbuzi, tutaendelea kuvumbua na kutoa huduma za kifedha na teknolojia ya kimataifa," alisema Karume.

Uzinduzi wa Benki ya NCBA Bank unafuatia idhini ya uunganaji iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na benki hiyo kuanza rasmi huduma zake Julai 8, mwaka huu. Ndani ya siku zijazo, benki hiyo ilisherehekea uzinduzi wa huduma zake kwenye matawi ambayo yamekwishaanza kazi kwenye mikoa ya Mwanza, Arusha na Zanzibar.



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akikata utepe kuzindua rasmi benki mpya ya NCBA, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Mkuu Mtendaji wa Benki hiyo, Margaret Karume na Mwenyekiti wa Bodi ya NCBA aliyemaliza muda wake, Sharmapal Aggarwal. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Prof. Mganilwa: Mradi wa SGR kukuza uchumi

Na Mwandishi Wetu

MKUU wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa, amesema kukamilika kwa mradi mkubwa wa reli ya kisasa ya SGR kutakuza uchumi wa kijiografia kwa nchi za ukanda wa kati hususani Rwanda, Burundi, Uganda na DRC.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea reli ya SGR akiambatana na Baraza la Uongozi la Chuo hicho mwishoni mwa wiki, Prof. Mganilwa alisema reli hiyo itakuwa nguzo kubwa kwa usafarishaji mizigo na abiria kwa nchi za ukanda wa kati (Central Corridor).

"Kukamilika kwa ujenzi wa mradi huu mkubwa na wa aina yake, utawezesha nchi za ukanda huu wa kati kufunguka kibiashara kwa kuwa usafirishaji wa bidhaa kwa nchi hizi utakuwa mzuri zaidi ya awali," alisema.

Aliongeza: "Reli ya SGR kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza na kipande kitakacho jengwa kutoka Isaka hadi Kigali nchini Rwanda na Musongati nchini Burundi itafungua ukanda wa kati wenye utajiri mkubwa wa madini na kilimo."

"Hivi sasa, zaidi ya asilimia 95 ya mizigo inayoondoka Bandari ya Dar es Salaam hubebwa na barabara na hivyo kufanya uharibifu kwa barabara. Kwa hivyo kujengwa kwa mradi wa reli hii kutaleta ongezeko kubwa la kubeba mizigo na abiria," alisema.

Aliongeza: "Tunatarajia kuona mradi wa SGR unapunguza gharama katika sekta zingine zinazohusiana na usafirishaji wa bidhaa na pamoja na usambazaji na hivyo kuboresha uchumi wa kijiografia kwa nchi za ukanda wa kati."

Alitabanaisha kuwa mradi wa reli ya kisasa utarahisisha kwa kiasi kikubwa adhima ya serikali kuwa nchi ya viwanda kwani usafirishaji wa bidhaa kwenda sokoni ama kutoka viwandani kwenye nje ya nchi kuwa wenye gharama nafuu na kwa wakati.

"Kupitia reli hii ya kisasa ya SGR, utalii kwa nchi yetu utakuwa kwa kasi kubwa ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa fursa za ajira, kwani watalii wataweza kusafiri kutoka Rwanda ama Burundi kuja Tanzania kwa muda mfupi sana kulinganisha na sasa," alisema.

Alisema kwamba ujenzi wa SGR utakuwa ni nguzo muhimu sana kwa nchi yetu ambayo ipo kwenye uchumi wa kati na ikiwa katika harakati za kufikia uchumi wa juu.

"Reli hii ya kisasa itaimarisha mazingira ya uchumi wa nchi ikiwa ni pamoja na kufungua milango ya uwekezaji kwa nchi za ukanda wa kati kwani gharama za uwekezaji zitapungua kutokana na kupungua kwa gharama za usafirishaji wa bidhaa," alisema.

Alisema NIT imeazimia kuanzisha kozi tano za usafiri wa barabara na reli ili kutosheleza mahitaji ya rasilimali watu katika miradi mikubwa katika sekta hii ikiwamo mradi huu wa reli ya kisasa ya SGR unaokuja.

"Chuo chetu kina mipango thabiti kabisa ya kuzalisha rasilimali watu ambayo itatosheleza sekta hii ya usafirishaji badala ya kuchukua watalaamu kutoka nje ya nchi," alisema.

Ilisema: "Tunakusudia kuzalisha wataalamu wa kutosha kwenye sekta hii ili miradi miradi mikubwa kama huu wa reli ya kisasa uweze kupata wafanyakazi wazawa."

Aliongeza kuwa kozi hizo mpya ambazo baadhi zitaanza kutolewa mwaka ujao wa masomo, zitatoa mafundi na wahandisi watakaokuwa na uwezo wa kufanya matengenezo ya reli hiyo ya SGR.

Tumeidhinisha kozi hizi kama hatua ya kuhakikisha kuwa mradi ujao wa SGR unasimamiwa na wenyeji, aliongeza Prof. Mganilwa.

## Baba jela miaka 30, bakora 12 kubaka mwanawe

Na Said Hamdani, LINDI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi, imemuhukumu mkazi wa Kijiji cha Mahiwa, Kata ya Nyangao, Maulidi Salum (25), kifungo cha miaka 30 jela, kuchapwa viboko 12 na kumlipa mlalamikaji fidia ya Sh. milioni 2 baada ya kupatikana na makosa mawili, likiwamo la kumpa ujauzito mwanawe wa kufiki ambaye ni mwanafunzi.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi, Maria Batraine, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka na mwenyewe kukiri makosa yake.

Hakimu Batraine akitoa hukumu kupitia Sheria ya Elimu kifungu cha 60 A fungu dogo la (3) Sheria ya Elimu alimhukumu kosa la pili la kumpa mimba na kukatisha masomo ya mwanafunzi huyo kifungo cha miaka 30 jela pamoja na kuchapwa viboko 12, na atakapomaliza kutumikia adhabu yake amlipe mlalamikaji fidia ya Sh. milioni 2.

Awali, Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mraakitoa, aliiambia Mahakama hiyo kwamba siku isiyofahamika Machi mwaka huu, mshtakiwa akiwa ni baba wa kufikia wa mkewe, alimbaka mtoto huyo (jina limehifadhiwa) mwenye umri wa miaka 13, ambaye anasoma Shule ya Msingi Mahiwa na kumpa ujauzito.

## Mpina akipigia debe kiwanda

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Kilimo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amesema kuna haja kubwa ya kukisaidia kiwanda cha Meat King Fish Distributor ili kiendelee kuchakata kwa nguvu zote nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo na mazao mengine ya mifugo.

Akizungumza jijini Arusha, Mpina alisema kufanya hivyo kunaboresha maisha ya wakulima, wafugaji na wavuvi.

Akizungumza baada ya kutembelea kiwanda hicho akifuatana na Kaimu Mkurugenzi wa Mikopo wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Jeremiah Mhada, Waziri Mpina ameitaka kuendelea kuvisaidia viwanda vinavyowasaidia wazalishaji mali wengi hapa nchini.

TADB imekuwa ikifanya kazi kubwa katika kuwasaidia wakulima, wavuvi na wafugaji wa nchi hii. Jitihada hizo ziendelezwe ili wadau wa sekta hizo wazidi kunufaika uboreshwaji wa mnyororo ya thamani katika sekta zao, amesema Waziri Mpina.

Alisema kuwa kuimarika kwa uzalishaji wa kiwanda hicho kunaleta manufaa kwa Watanzania kwani kunapunguza ukosefu wa ajira kwa Watanzania na kunaimarisha ajira za wafugaji na kuwafanya wawe na uhakika wa soko la bidhaa zao.

"Uimarishwaji wa uzalishaji katika kiwanda hiki utasaidia kutengeneza ajira mpya na kuimarisha ajira za zamani kwa wadau wa kilimo, ufugaji na uvuvi," alisema na kuongeza kuwa uchumi wa viwanda hautakuwa na maana kama sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi hazitafanyiwa mageuzi makubwa.

ama
ALHAMISI AGOSTI 20, 2020
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

**Zahanati mpya inavyofuta vifo vya wajawazito Halmashauri Kahama**



Ukurasa 13

**MABINTI SHULENI ...**
RC Rukwa katika mpango kabambe kumaliza mimba zilizomchefua JPM



Ukurasa 14

**ALICHOTANGAZA PUTIN... Chanjo mpya ya corona Russia,yawanyima usingizi Magharibi**

AFYA

# Hii hapa sumukuvu, madhara yake na jinsi inavyodhibitiwa

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), ni taasisi yenye dhamana ya kusimamia na kudhibiti usalama wa chakula nchini, ambayo imejumuika na mataifa katika kuadhimisha Siku ya Chakula Salama Duniani, kila siku ya Juni 7 ya mwaka.

Usalama wa chakula waweza kuwa mtazamo mpana wa chakula kuwa salama, maana mlo ni jambo moja na usalama wake ni jingine. Hapo ndipo kunaibuka dhana ya kuwapo sumukuvu katika vyakula kutoka shambani.

Hapo kuna umuhimu kujua, hiyo ni nini?

Ni sumu zinazozalishwa na kuvu au fangasi wa makundi mbalimbali, wanaoota zaidi kwenye mazao ya chakula.


Sumukuvu huzalishwa kwenye mazao, zikiwa katika hatua mbalimbali kama vile, shambani, baada ya kuvunwa,wakati wa kusafirisha au uhifadhi.

Waathirika wakuu ni vyakula aina ya nafaka na mbegu za mafuta. Hapo unataja mahindi na karanga, ambazo ni mlo maarufu katika jamii ya Watanzania.

Pia, sumu hizo huwa hazikosekani kwenye mazao ya biashara. Hivyo, panapojitokeza suala la sumu kuvu ndani yake, ni simulizi ya madhara yanayoathiri biashara ya mazao hayo

Sumukuvu zinapokuwepo kwenye mazao au bidhaa, zina kawaida ya kuendelea kubaki, hata baada ya chakula kupikwa au kusindikwa.

Aina ya kuvu wanaosababisha sumu zinatajwa zipo nyingi, wanaoweza kushambulia mazao, wanaotajwa wapo wa makundi matatu, yanayotajwa kwa majina ya Aspergillus, Penicillium na Fusarium.



Bidhaa kilimo zinazoweza kuathiriwa na sumukuvu. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Mahindi yaliyoathiriwa na sumukuvu.

Kitaalamu, hao ndio wahusika na kuzalisha sumu kuvu kwenye mazao ya nafaka na mbegu za mafuta na zipo aina nyingi za sumukuvu zinazozalishwa na kuvu tofauti.

Uchafuzi wa sumu kuvu katika mazao ya chakula pamoja na kiwango cha madhara ya kiafya kwa binadamu yatokanayo na sumukuvu nchini, zaidi inatajwa kuwa ni 'aflatoxins' na 'fumonisins'ndiyo tatizo zaidi.

Kumbuka uwepo wa kuvu na kuzalisha sumukuvu unategemea na hali ya hewa ya mahali husika, hivyo maeneo tofauti huweza kuwa na kiwango na aina tofauti za kuvu.

Dalili za uchafuzi wa sumukuvu kwenye mazao ya chakula zinapokuwepo kwenye mazao au bidhaa, hazionekani kwa macho, pia huendelea kubaki hata baada ya chakula kupikwa au kusindikwa.

Mazao yaliyochafuliwa na sumukuvu, ishara zake ni pamoja na ukungu, harufu ya uvundo, nafaka kutengeneza vumbi, nafaka kugandamana, nafaka kubadilika rangi na kuwa na weusi.

Mahindi na karanga ni mazao muhimu ya chakula ambayo hushambuliwa na fangasi wanaozalisha sumukuvu kwa wingi na mazao yaliyoshambuliwa na kuvu sumukuvu inavyoweza kumfikia mlaji.

**ATHARI ZAKE**

Hatari ya mlaji kupata sumukuvu, ni pale endapo, atakula chakula kilichochafuliwa na sumu hiyo, au atakula mazao yanayotokana na mifugo kama vile maziwa, endapo mifugo italishwa chakula kilichochafuliwa na sumukuvu. Mfano wa vyakula hivyo, ni mashudu au nafaka mbovu.

Mtoto atakaponyonya maziwa ya mama aliyekula chakula kilichochafuliwa na sumukuvu, na inaangukia hatari ya lishe hiyo yenye sumu.

Ulaji wa vyakula vilivyochafuliwa na sumukuvu, huweza kusababisha madhara mbalimbali ya kiafya na yanajitokeza ndani ya muda mfupi au baada ya muda mrefu, kutegemea na kiasi cha sumu kwenye mlo, kiasi cha chakula kilichochafuliwa, pamoja na umri na hali ya afya ya mlaji.

Madhara yanayotokea ndani ya muda mfupi, hujitokeza pale kiasi kikubwa cha sumukuvu kimeliwa. Hapo unataja kuathirika kwa ini, figo, mfumo wa fahamu na kupunguza uwezo wa damu kuganda na hata kifo.

Athari za sumukuvu kiuchumi, inashuhudiwa biashara ndani ya nchi, kikanda na kimataifa, ambao uchafuzi wa sumukuvu unasababisha matatizo mtambuka.

Hapo unataja kukataliwa bidhaa za chakula zilizozidi viwango vya sumukuvu vinavyokubalika katika soko, kukosa mapato, kupungua akiba ya chakula.

Kitaalamu ni kwamba chakula kilichochafuliwa zaidi ya kiwango kinachoruhusiwa, huwa hakifai kwa matumizi ya binadamu na mifugo, hivyo kinapaswa kuharibiwa.

Pia, lipo suala la kuongezeka gharama za matibabu na kupungua nguvu kazi na uzalishaji mali.

**UDHIBITI**

Wadudu wasipodhibitiwa huongeza unyevu na joto katika ghala ambavyo huchochea kuvu kuzaliana na kuzalisha sumukuvu.

Viuatilifu visipotumiwa kwa usahihi vinaweza kuathiri afya ya mlaji, hivyo inapaswa kuzingatia matumizi ya viuatilifu kwa kiwango sahihi na muda mazao yaliyowekwa viuatilifu yanahifadhiwa kabla ya kuruhusiwa kwa matumizi.

Namna mojawapo muhimu ya kudhibiti sumukuvu wakati wa kuandaa mazao kwa ajili ya chakula, mhusika anapaswa kupeta, kuchambua na kuondoa taka, mbegu hafifu, zilizopasuka na zilizooza.

Pia, kwa zilizobadilika rangi na zilizoharibiwa na wadudu, kazi kuu ni kuziosha, kuondoa vumbi, udongo na punje dhaifu, kisha mahindi yanayokobolewa kabla ya kusaga na baada ya kusaga mahindi hayo yanahifadhiwa kwenye chombo safi kisichoruhusu unyevu kuifikia.

AFYA

# Zahanati mpya inavyofuta vifo vya wajawazito Halmashauri Kahama

## •Mganga Mkuu: Nina miaka 3, sijaona vifo



Jengo la Zahanati ya Kijiji cha Nduku, katika Halmashauri ya Mji Kahama, Shinyanga kabla ya kuanza kutumika. **PICHA: SHABAN NJIA.**

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

KATA ya Kinaga ni kati ya zinazozunda Halmashauri ya Mji wa Kahama Mkoani Shinyanga. Mahali hapo kuna zahanati moja isiyotosheleza mahitaji na kusababisha wengi kujifungulia majumbani kwenye mazingira hatarishi.

Kata hiyo ilikuwa na zahanati moja ya Kinaga iliyojengwa tangu mwaka 1985, ilihudumia vijiji 10 kutoka Kata ya Mwanase na Kinaga, kabla ya kata kugawanywa kutoka Halmashauri ya Msalala na kuhamia Halmashauri ya mji Kahama. Wakati huo, mbunge wao alikuwa Ezekiel Maige.

Baada ya kugawanywa na kubaki vijiji vitano, bado zahanati iliyokuwapo haikutosheleza mahitaji ya wananchi wa kata husika kupata matibabu.

Wananchi kwa kushirikiana na diwani aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020. Waliungana kuchangisha fedha kila kitongoji na hata walifanikiwa kujenga zahanati mpya ya Nduku.

**HALI ILIVYOKUWA**

Angelina Mabula, mkazi wa kijiji na kata ya Kinaga, katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, anasema katika zama zilizopita za kuwa na zahanati moja ya Kinaga, wananchi wa vitongoji vya Iguno, Igumbili, Nyang'ombe, Nyahungwe na Bukomela walishindwa kufika kupata matibabu.

> **Mwaka 2000 wakati nikiwa kwenye mstari aliletwa mjamzito kwenye baiskeli akiwa amechoka na uchungu ukimsumbua sana, kwa sababu alichelewa kufika kituoni. Alipoteza maisha pamoja na mtoto," anasimulia Angelina.**

Anasema wagonjwa wengi hasa wajawazito walilazimika kujifungulia majumbani, wakipata huduma hiyo kutoka kwa ama waume au majirani zao, wasio na elimu, pia vifaa vya huduma hiyo.

"Mwaka 2000 wakati nikiwa kwenye mstari aliletwa mjamzito kwenye baiskeli akiwa amechoka na uchungu ukimsumbua sana, kwa sababu alichelewa kufika kituoni. Alipoteza maisha pamoja na mtoto," anasumulia Angelina.

Scola Peter, anasema walilazimiaka kutembea kilometa saba kufika zahanati ya Kinaga, safari walioianza alfajiri kuwahi msongamono uliokuwepo kuhudumia kata za Mwanase na Kinaga.

Kuna simulizi ya Roza Bundala, anasema wengi hawakuona umuhimu wa kuhudhuria kliniki kwanza kwa zahanati kuwa za mbali, msongamano mkubwa wa wagonjwa kuchukua uamuzi kujifungua majumbani, pasipo kujali hataria.

Mama Pili Maziku, anasema vifo vya kinamama wajawazito na watoto, vilikuwapo kwa wakati huo hasa wajawazito kujifungua njiani, walipokiwa wakielekea zahanati Kinaga, walikosa usaidizi wa kujifungua na kujizalisha mwenyewe.

"Kama mmeo hana uwezo wa kununua baskeli ilikuwa vigumu kufika zahanati ya Kinaga kwenye matibabu na ukilazimika kutembea kwa miguu alifajiri unafika kituoni saa mbili na kutoka jioni," anasema Maziku.

Anafafanua, ilikuwa chanzo cha kukosekana umuhimu wa wajawazito kuhudhuria kliniki, kujua mtoto kama yuko salama au la.

Angelina, anampongeza aliyekuwa diwani wao na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Mary Manyambo, kwa kuwahamasisha wananchi kuchangia na kujenga zahanati nyingine mpya ya Nduku.

Ni mchango uliomhusisha kila mwananchi wa kitongoji kuchanga alichokiweza, kama vile mawe, mchanga, saruji au matofali na aliyekuwa mbunge, Ezekiel Maige, kuchangia mifuko 100 ya saruji kutoka fedha za Mfuko wa Jimbo.

Kai ya ujenzi inaelezwa ilianza mwaka 2013 na kukamilika mwaka 2017, sasa ikitoa huduma za kiafya kwa karibu hasa wa vitongoji vya Iguno, Igumbili, Nyang'ombe, Nyahungwe na Bukomela, hata kupunguza msongamano wa wagonjwa Kinaga.

Christina Christian, anasifu sasa huduma ya mama na mtoto kwenye zahanati za Nduku na Kinaga, bila ya usumbufu kama ilivyokuwa awali.

"Kinamama tunahudhuria kiliniki kwa wakati na tunajifungulia kwenye vituo vya afya, kutokana na kutusogezea huduma karibu," anasema Christina, huku akiungwa mkono na mkazi, Jackson Elias, kuwa adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta matibabu.

**UONGOZI HALMASHAURI**

Aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, kipindi kilichopita, Mary Manyambo, anasema wakati anaingia madarakani, vipaumbele vyake ilikuwa kujenga zahanati kila kijiji ambapo mpaka sasa ameshajenga zahanati ya kijiji cha Nduku.

Anasema, kabla ya kuvunjwa kwa Mabaraza ya Madiwani, alishirikiana na wananchi wa vitongoji, vijiji na kata kujenga maboma mawili ya zahanati ya kijiji cha Ubilimbi na Igunwa, ili kusogesha huduma za afya kwa wananchi na kudhibiti vifo vya kinamama na watoto.

Dk. Lucas David, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Kahama(TMO), anasema tangu alipofika Kahama mwaka 2017, wakati zahanati ya Nduku inaanza kutoa huduma ya afya, hakujawahi kuripotiwa mkasa wa vifo vya wajawazito, watoto magonjwa wengine.

Anasema, awali kabla ya kujengwa zahanati walikuwa wakitumia zahanati moja ya Kinaga na kusababisha msongamano wa wagonjwa, lakini sasa hakuna tena msongamano wa wagonjwa.

Dk. David anasema kila mwananchi anatakiwa kuwa na bima ya CHF, ili kuwapunguzia gharama za matibabu kwenye vituo vya afya au zahanati.

Anasema, waratibu wa bima ya afya iliyoboreshwa CHF wako kwenye vijiji, kata na wilaya wakitoa elimu ya umuhimu husika, ikue dhana na kuwakatia bima wananchi wenye uhitaji kwa gharama ya Sh. 30,000 peke kwa familia ya watu sita.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya mji wa kahama Anderson Msumba anasema kuwa, ukamilishaji wa zahanati ya kijiji cha Nduku kata ya Kinaga umegharimu kiasi cha Sh. Milioni 52.9, Halmashauri ilitoa kiasi cha Sh. Milioni 14.2, serikali kuu Sh. milioni 30.2 na nguvu za wananchi Sh.milioni 8.8.

Anasema kuwa lengo la kujenga kwa zahanati hiyo ya kijiji, ni kuwaondolea adha wananchi kutembea umbali mrefu kufika katika zahanati ya kata ya Kinaga na hospitali ya Mji wa Kahama, kutafuta matibabu kama moja ya kupambana na vifo vya akina mama wajawazito na watoto kwa wakati huo.

**SHIDA ZILIZOKO**

Yasinta Masele, Mkazi wa kijiji cha Nduku, anasema wamekuwa wakikosa matibabu kwenye zahanati ya Nduku na Kinaga, wanapokosa kadi za Bima za Afya za (CHF), hata wakaingia katika gharama kubwa zaidi.

Anasema, mwitikio wa wananchi kukata bima za afya ni mdogo na wengi hawana elimu ya umuhimu wake, huku hasara wanazopata ni baadhi yao wanaokosa matibabu kwa kutokuwa na bima hiyo na fedha za kumuona daktari.

Raphael Stephen, anaongeza kuwa, wengi wanaopata adha hizo ni wazee, wakilinganishwa na vijana.

Anasema kuwa, lengo la kujenga kwa zahanati hiyo ya kijiji ni kuwaondolea adha wananchi kutembea umbali mrefu kufika katika zahanati ya kata ya Kinaga na Hospitali ya mji wa kahama kutafuta matibabu kama moja ya kupambana na vifo vya akinamama wajawazito na watoto kwa wakati huo.

AFYA

SHIDA ZA MABINTI SHULENI

# RC Rukwa katika mpango kabambe kumaliza mimba zilizomchefua JPM

- Alinyoosha kidole kuchezea ufadhili wake
- Mkoa kinara wa 14, jirani yake Katavi 11
- DEO: Shida iko kote, sekondari na msingi

**Na Nebart Msokwa, aliyekuwa Sumbawanga**

RUKWA imo katika orodha ya mikoa nchini inayokabiliwa na tatizo la wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, kukatishwa masomo kwa kupata mimba.

Ni mambo yanayotajwa kukatisha ndoto za maisha ya vijana shuleni, kuishia njiani.

Takwimu ya Sensa ya Hali ya Idadi ya Watu na Afya nchini (TDHS-MIS) ya mwaka 2015/2016, inaonyesha asilimia 29 ya kinamama wenye umri kati ya miaka 15 na 19 mkoani humo ama wamezaa au ni wajawazito.

Taarifa inabainisha mkoa kushika nafasi ya 14 nchini kwa tatizo la mimba za utotoni, huku majirani zao wa Katavi wakiwa mbele kwa asilimia zaidi ya 11.



Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo (aliyeshika mkasi) akikata utepe kuashiria kuzinduliwa rasmi kwa Mpango Maalum wa Kimkoa Kukabiliana na Mimba za Utotoni. **PICHA ZOTE: NEBART MSOKWA.**

**MGANGA MKUU**

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Dk. Boniface Kasululu, anasema katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2017 hadi Agosti mwaka jana, kuna wanafunzi 722 walipata mimba

Ni kauli aliyoitoa kwenye uzinduzi wa Mkakati wa Kutokomeza Mimba za Utotoni, Dk, Kasululu, akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kuandaa Mpango huo anasema kati ya waliopata mimba katika kipindi hicho, 551 walikuwa na shule za sekondari na 171 shule za Msingi.

Anasema, mkoa haukuwa na mpango wa kutafuta na kushughulikia taarifa za mimba, kuna uwezekano takwimu hizo kuwa za chini kuliko uhalisia.

Dk. Kasululu anasema, matukio ya mimba za watoto yanayoripotiwa polisi yanaongezeka kila mwaka, akitoa mfano katika mwaka 2018, yaliongezeka kufikia 247 kutoka 72 za mwaka 2016.

"Takwimu pia zinaonyesha karibu robo ya kinamama wanaohudhuria hudhurio la kwanza katika kliniki ya wajawazito, yaani asilimia 24, wana umri wa chini ya miaka 20," anasema Dk. Kasululu.

Anasema ongezeko ni zao la jamii kuchukulia suala la mimba za utotoni, jambo la kawaida na hivyo kutochukua hatua za kukabiliana nalo.

Pia, Dk. Kasululu anataja umaskini miongoni mwa wananchi na kutowajibika wazazi na viongozi katika ulinzi wa msichana, ikiwarahisisha kuingia kwenye mitego ya mimba.

Vilevile, anataja elimu duni katika jamii, mila, desturi, imani zinazomkandamiza mtoto wa kike, malezi hafifu, kuporomoka maadili ya kijamii, jamii, uelewa mdogo kuhusu sheria zinazosimamia uhusiano wa watoto.

**JPM AKERWA**

Alipokuwa ziarani Mkoa wa Rukwa Oktoba, mwaka jana, Rais Dk. John Magufuli, hakuficha anavyochefushwa na takwimu za wanafunzi wanaopata mimba na kukatishwa masomo, hata akawaachia maagizo mazito viongozi wa mkoa kuwajibika na udhibiti huo.

Katika hotuba yake kwa wakazi wa Sumbawanga, aliwakejeli wanaohusika na kusababisha mimba, kwamba "wakati serikali ikikazana kutoa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa elimu bila malipo, wanaume wa mkoa huo (Rukwa) nao wamekazana kuwapa mimba wanafunzi."

"Kwa taarifa nilizonazo ni kwamba, kwa mwaka jana pekee (2018), wanafunzi 229 walipata mimba, sisi tunatoa fedha nyingi kwa ajili ya kuendesha elimu bure. Ninyi hapa Rukwa mnatoa mimba bure, sasa nitoe wito kwa viongozi wa mkoa, wilaya na vyombo vya dola mzingatie sheria," aliagiza.

Ni ujumbe uliowarudia na wanafunzi kuacha 'viherehere' vya kujiigiza katika yanayowahatarisha kuangukia katika kujitwuisha mimba na kujikatisha masomo.

**RC ALIVYOJIPANGA**

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo maarufu 'Chifu' anasema, kwa kushirikiana na wadau wake likiwemo, shirika la Plan International, watekelezaji mradi wa 'Uzazi Salama' mkoani humo, wameandaa mkakati wa miaka mitano, ulioanza mwaka huu.

Anasema, ni mkakati unaowashirikisha wadau wakiwamo wazazi, walezi, viongozi wa serikali na taasisi zisizokuwa za kiserikali, zinatetea haki za watoto.

Wangabo anasema, Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 na marekebisho yake ya mwaka 2016, inamlinda mtoto na kwa kuharamisha mambo yote yanayoweza kumkatisha kuendelea na masomo.

Vilevile, anasema Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2016, inaainisha haki zake ikiwamo ya kupata elimu na wajibu wa wadau mbalimbali kuhakikisha wanalinda haki za mtoto.

Pia anasema mwaka 2016, serikali iliandaa mpango kazi wa kitaifa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa miaka mitano, kuanzia mwaka 2017 mpaka 2022, ikiwa ni pamoja na kukomesha mimba za utotoni.



Baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wa Mkoa wa Rukwa, wakiwa kwenye maandamano ya kupinga ukatili dhidi yao, wakati wa kuzindua Mipango wa Mkoa Kukabiliana na Mimba za Utotoni

**MKAKATI MKOA**

Anasema, mkoa Rukwa kwa kushirikiana na wadau wake, ilianzisha mpango wake wa kukomesha ukatili dhidi ya watoto na mimba za utotoni, ili watoto wapate fursa stahiki bila ya kukatizwa.

"Mkakati huu tuliuzindua na kuukabidhi kwa kila Mkuu wa Wilaya, ili wautekeleze kwenye wilaya zao wakishirikiana na wadau wengine, mkakati unawashirikisha pia viongozi wa dini, walimu, wazazi na vyombo vya dola," anasema Wangabo.

Mkuu wa Mkoa anataja moja ya visababishi vya mimba, ni wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda na kutoka shuleni, kwani kuna baadhi ya vijiji havina shule za msingi na baadhi ya kata hazina shule za sekondari.

Anataja takwimu za Rukwa kwamba una jumla ya vijiji 339 na kata 97 Hata hivyo, jumla ya kata 25 hazina shule za sekondari, hivyo watoto wanalazimika kwenda kusoma shule za kata zingine na katika shule hizo, zenye mabweni na hoteli ni chache zaidi.

Wangabo anasema, viongozi wa vijiji na kata zilizokosa shule, wameelekezwa kuanza ujenzi wa shule na kwa viongozi wa kata zenye shule, waanze kujenzi mabweni ili wanafunzi wao wahame kutoka nyumba za kupanga jirani, maarufu za kupanga jirani'mageto'.

**MBUNGE ASHUHUDIA**

Aliyekuwa mbunge wa Viti Maalumu Mkoa Rukwa, Aida Khenan (Chadema), anasema ni miongoni mwa wasichana waliowahi kukatishwa masomo, kwa kupata mimba akiwa shuleni kwenye mkoa huo.

Anasema kutokana na mwamko wa elimu wa wazazi wake, walimrudisha shuleni baada ya kujifungua na akafaulu vizuri masomo yake na kuendelea mpaka elimu ya juu iliyomuwezesha kufikia hatua ya kuwa mbunge.

Anawataka wasichana kuepuka kushiriki ngono wakiwa bado wanaendelea na masomo kwa maelezo kuwa kwa jinsi sheria za nchi zilivyo hawawezi kuendelea na masomo kwenye shule za serikali wakipata mimba.

"Mimi nilipata mimba nikiwa kidato cha tatu, lakini hiyo haikuwa sababu ya wazazi wangu kunikatia tamaa, walipambana na mimi mpaka nikasoma na kumaliza kidato cha nne nikiwa bado mzazi, sasa hiyo inategemea mwamko wa wazazi na kipato," anasema Aida.

Anawataka wazazi wa wasichana waliokatishwa masomo, lakini bado wanahitaji kusoma wawapeleke shuleni, ili wafikie ndoto zao ambazo zinakatishwa na walaghai.

AFYA

## ALICHOTANGAZA RAIS PUTIN...

# Chanjo mpya ya corona Russia, yawanyima usingizi Magharibi

**Na Michael Eneza**

RUSSIA imekuwa ya kwanza kutangaza ugunduzi wa chanjo ya ugonjwa wa corona, kufanya majaribio na kuanza kutumia kwa wengi, dawa ambayo imepewa jina la 'Sputnik V.'

Hiyo ni kumbukumbu ya jinsi Umoja wa Jamhuri ya Kisovieti (USSR), ulivyotangulia kupeleka mtu angani mwaka 1957, kazi iliyofanywa na Meja Yuri Gagarin.

Rais Vladimiri Putin, alitangaza mafanikio na kuwaambia wananchi katika hotuba ya televisheni, kuwa binti yake ni mmoja wa waliochanjwa kwa dawa hiyo, ila wachunguzi habari waliongeza hakusema ni binti yupi.

Ni tangazo lililochangia hatua nyingine ya ushindani kati ya nchi za Magharibi. Wiki chache zimepita, tangu mashirika ya kijasusi ya Marekani, kusema Russia ilikuwa inatafuta vyanzo vya kimtandao (kwa kupenya katika hifadhi za kampuni zinazotafitii chanjo), mara moja inatangazwa kuwa tayari chanjo ipo.

Hiyo ina maana, taarifa za ujasusi hazikupatikana mapema, ila hadi ama Russia inafikia chanjo yake ya kwanza au Marekani ilichelewa kutoa tahadhari kama hiyo, ikifanya ukaguzi wa kwanza. Russia ilikanusha uvumi huo.

Maofisa serikali ya Russia, wanatazamia chanjo itaaanza kutolewa kwa umma wa walimu na wafanyakazi wa sekta za afya, walio hatarini kuambukizwa virusi vya ugonjwa huo.

Tangazo la kuanza kutumia chanjo hiyo bila kuifanyia majaribio kwa wengi kama taratibu za kitaaluma zinavyotaka, inaifanya isikubalike katika hatua yake ya sasa, iwe kwa nchi za Magharibi au Shirika la Afya Duniani (WHO).

Maofisa wa WHO, wanasema wanafuatilia kwa karibu kinachoendelea Russia, lakini hapakuwa na mpango wa kuitambua chanjo hiyo.

Eneo jingine la ukosoaji tangazo la upatikanaji chanjo Russia, hapakuwapo machapisho na kupitia wataalamu wenza, kuhusu kinachofanyika katika Taasisi ya Gamaleya, iliyotafiti kufikiwa chanjo tarajiwa.

**UKWEPAJI HOJA**

Wafuatiliaji taarifa hizo katika mashirika ya nje, mathalan, gazeti la Washington Post la Marekani, walipata shida ya kulieleza hilo, kwani taasisi hiyo ilikuwa inajibu maswali ya utafiti wa chanjo, yaelekezwe katika Wizara ya Afya nchini humo, huku maofisa wizara wakikataa kutamka lolote.

"Watalaamu wa nje, walitaka kujua ni majaribio gani ya 'hatua ya tatu' (jaribio la watu wachache, vikundi na makundi ya watu) kabla ya kupitisha chanjo hiyo itumike," inafafanua.

Hilo lilihitimishwa kwa wakosoaji wakitaka kupitishwa chanjo bila ya kupitia hatua tatu, tena zionyeshe mafanikio hatua moja kwenda nyingine. Ni mchezo wa kubahatisha, ikifananishwa na kamari maarufu nchini humo 'Russian roulette.'

Huo ni mduara kuzungusha gurudumu, halafu litakaposimamia ndiyo pesa zinamwagika ni maelezo ya baadhi ya wataalamu kutoka taasisi pinzani ndani ya Russia au walio na uhusiano na nchi hiyo, licha ya kufanya kazi au kuishi nchi za Magharibi,

Wanasema, suala ni kutafuta sifa kwa ajili ya Russia kama taifa, dhamira inaainishwa na kutolewa jina la 'Sputnik V' au alama za ubingwa wa Russia kihistoria.

Kutumia jina na jinsi Russia wakati huo ilivyoongoza kupeleka mtu angani, kuna uhusiano wa karibu na hali ya sasa, kwa maana kuwa na utafiti wa chanjo unaohitaji kuhakikishwa nguvu zote dhidi ya madhara au kutokuwa na ufanisi.

Ni jambo linalochukua muda mrefu, kutokana na mlolongo wa hatua za uthibitishaji kitaaluma na kiutawala, wakati Russia inapitisha uamuzi haraka zaidi, kwa sababu ya kukosekana mgawanyo wa kina, kuhusu madaraka.

Unatolewa mfano, pale panapokea tatizo mbele ya safari, hakuna hitaji la kuchunguza ilikuwaje chanjo ikapitishwa, kwani dhamira njema ya walio madarakani imeshathibitishwa.

Binti wa Rais, naye alishiriki chanjo kama mmoja wa waliotumia hatua za kwanza kuanza kutumika mahitaji pana ya umma.

Ilisikika pia, China imesharuhusu chanjo moja kuanza kutumika, ila itawahusu wapiganaji wa Jeshi la Ulinzi pekee, kabla ya kuhakikishiwa kitakwimu inafaa kutumika kwa mahitaji pana zaidi ya taasisi maalum kama jeshi.

**WATAFITI WALIVYO**

Makamu Mtendaji Mkuu Taasisi ya Utafiti wa Uhusiano wa Kimataifa jijini Washington, Mayekanik Stephen Morrisonam, anasema, huko ni kubadili kanuni, ni kukata kona.

Linatajwa ni tukio kubwa la linalianza na Rais Putin, kwani anahitaji ushindi, katika' (katika suala hilo). Wengi walikubaliana naye.

Ilionekana kuwa jitihada za Russia siyo tu kutangulia, ila kuhakikisha kuwa ina chanjo yake yenyewe na haitegemei mafanikio katika sekta hiyo maalum yanayofikiwa katika nchi za Magharibi, kwani kihistoria ina uhusiano mbaya na nchi hizi.


Baadhi ya wataalamu wameanza kuingia wasiwasi kuwa nchi kubwa duniani zitatumbukia katika dimbwi la 'uzalendo wa chanjo ya corona,' ambako kila nchi itatumia yake kuepuka gharama kubwa ya kuagiza chupa za chanjo, hasa kutoka Marekani, China au kwingine.

Morrison anatikisa kichwa akitafakari hali hiyo na kuhofia kuwa inaweza kuleta tatizo jingine, akikumbushia kuwa Russia kupitia taasisi hiyo kati ya mwaka 2015 hadi 2018, ilitengeneza chanjo ya ugonjwa la Ebola ambayo hadi sasa haijatambuliwa na WHO kwani majaribio yake na mafanikio ni haba.

Baadhi ya wanaochunguza maendeleo ya chanjo tarajiwa kwa karibu zaidi, wanasema Russia inatumia dozi mbili za kuingizwa 'virusi poa', vinavyoitwa 'adenoviruses' na ambavyo huganda katika 'protini pembe' ya corona hivyo 'kufisha' au kubutisha nguvu zake za kupenya katika kuta za chembe hai mwilini.

Mwelekeo huo uliotumiwa katika chanjo hiyo ya awali ya Ebola, inayotumiwa na kampuni kama Johnson&Johnson katika utafiti wa chanjo ya corona, kampuni ya utafiti ya China, Cansino Biologics na hata Chuo Kikuu cha Oxford nchini Uingereza.

Ila kuna mtafiti anayeifahamu Taasisi ya Gamaleya vizuri, akieleza kuna uhakika mkubwa wa Russia kuhusu ufanisi tarajiwa wa chanjo hiyo, kiasi kwamba ofisa huyo ambaye yuko Russia, ameitumia chanjo hiyo na familia yake, ikiipa hadhi kuwa na maana na uhakika kuhusu ubora wake.




Dawa zitakazotumika kwa ajili ya chanjo ya corona. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Askari wa Russia akipata huduma ya chanjo ya majaribio dhidi ya ugonjwa wa corona.





# Mradi wa viwanda waokoa milioni 300/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema mradi wa kuimarisha viwanda kwa kuongeza tija katika uzalishaji na ubora wa bidhaa zinazozalishwa (KAIZEN), umeokoa Sh. milioni 300 ambazo zingetumika visivyotarajiwa viwandani.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe, alipokuwa akizindua Mpango wa Kitaifa wa uongezaji endelevu wa ubora na tija katika sekta ya uzalishaji viwandani kwa mwaka 2020 hadi 2030, uliosimamiwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA). Akizindua mpango huo katika maadhimisho ya Siku ya KAIZEN, alisema katika mwaka 2019/20 wizara ilifanya tathmini ya hali ya utekelezaji wa mradi wa KAIZEN, na kubaini kuna ongezeko la ubora na tija kwa bidhaa za viwandani kutokana na usimamizi bora ambao umeokoa kiasi hicho cha fedha.

"Tulifanya mafunzo kwenye viwanda ya matumizi ya falsafa ya KAIZEN ambayo yameokoa kiasi cha Sh. milioni 300 ambazo zingetumika ndivyo sivyo," alisema.

Aidha, Prof. Shemdoe alisema Rais John Magufuli ameonyesha wazi kuwa anatumia falsafa ya KAIZEN katika miradi mingi inatekelezwa kwa fedha za serikali.

Hata hivyo, alisema wizara imeandaa, mpango huo wa miaka 10 wa kueneza falsafa ya KAIZEN nchi nzima ambapo itasaidia kuweka mikakati mizuri ya kushawishi na kuvutia sekta nyingine kufanya kazi kwa bidii.

"Tupo uchumi wa kati wa chini tunatarajia kufikia uchumi wa juu, ni matarajio yangu ifikapo 2025 tutakuwa tumefika juu, na hili liwe lengo letu, na kupitia KAIZEN tutafika, uchumi wa nchi utakwenda mbele kama tutazalisha bidhaa kutoka kwenye viwanda vyetu," alisema.

Kadhalika, katibu huyo alisema nchi 16 zinatarajia kushiriki kwenye mashindano ya KAIZEN Tanzania na viwanda viwili vya hapa nchini vitashiriki kuonyesha bidhaa vinavyozalisha kwa nchi hizo.

"Viwanda hivyo vijiandae ili tuzo tuliyoipata isitoke nje ibaki hapa hapa nchini, jiandaeni vizuri maana ni tukio la kitaifa na tunatakiwa tunufaike nalo kiuchumi," alisisitiza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO), Prof. Sylvester Mpanduji, alisema kuwa wamehamasisha matumizi ya mfumo wa KAIZEN kwenye ofisi zao hivyo kuwataka wadau wengine kutumia maana una manufaa mengi.

"Mpaka sasa SIDO imehudumia kongani 56 kwa kushirikiana na JICA, ambapo viwanda 479 ambavyo vimeajiri Watanzania 3,978," alisisitiza.

**Rais John Magufuli ameonyesha wazi kuwa anatumia falsafa ya KAIZEN katika miradi mingi inatekelezwa kwa fedha za serikali.**

# Askofu aonya matusi kwenye kampeni

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

ASKOFU wa Kanda ya Kati wa Kanisa la PHAM, Julius Bundala, amewataka wagombea wa nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu, kuepuka kutumia lugha za matusi wakati wakinadi sera zao ili zikubalike kwa jamii.

Askofu Bundala alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifunga mkutano wa wanawake wa kanisa hilo, Jimbo la Kongwa mkoani Dodoma.

Alisema Watanzania wanahitaji kusikia sera za vyama jinsi watakavyowatumikia wananchi katika kutatua kero zao na si lugha hizo za kukashfiana.

Aliwahimiza wanawake hao kuwaombea wagombea ili wanadi sera zao bila kutoleana maneno ya matusi.

"Hakikisheni mnawaombea wagombea wetu kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu ili uwe wa amani na utulivu na hatimaye wapatikane viongozi watakaokubalika na Mungu na Watanzania wote," alisema.

Katika hatua nyingine, Askofu Bundala aliwashauri wakulima wa mikoa ya kanda ya kati kutumia mbegu za muda mfupi ili kuendana na kiwango cha mvua zinazonyesha kwenye maeneo hayo.

Alisema kuwa wakulima wanatakiwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa kilimo ili kujipatia chakula cha kutosha kwa kutumia mbegu za muda mfupi, huku akiwaasa kuachana na kilimo cha mazoea kisichokuwa na tija kwao.

"Panapohitajika kulimwa mtama palimwe mtama, na panapolimwa alizeti palimwe alizeti na hata kwenye kulima mahindi ni hivyo hivyo, hii itawasaidia kujikwamua kiuchumi kwa kuwa watakuwa na chakula cha kutosha," alisema.

Aliwataka wanawake hao kufanya shughuli za uzalishaji ili kujikwamua kiuchumi.

**Watanzania wanahitaji kusikia sera za vyama jinsi watakavyowatumikia wananchi katika kutatua kero zao.**




Mfanyabiashara wa matikiti, maji Mzee Walangolango, akiyapanga wakati akisubiri wateja katika soko kuu la Majengo, jijini Dodoma, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mikakati 5 usalama wa chakula yatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetaja mikakati mitano ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini unaendelea kutengemaa ikiwamo kuboresha mifumo ya uhifadhi wa mazao ya chakula kwa ngazi zote.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alitaja mikakati hiyo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya uzalishaji mazao ya chakula kwa msimu wa mwaka 2019/2020 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2020/21.

Alisema serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha usalama wa chakula unakuwapo.

Alitaja mkakati mwingine ni kufanya maandalizi mapema ya ununuzi wa pembejeo za kilimo kwa ajili ya msimu wa 2020/21.

"Mikakati mwingine ni kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa mazao ya chakula kuanzia ngazi ya kaya," alisema.

Kadhalika, alisema mkakati mwingine ni kuhamasisha kilimo cha umwagiliaji na kutumia fursa ya uwapo wa mabonde yenye unyevu kupanda mazao yanayokomaa kwa muda mfupi, ili kuongeza upatikanaji wa chakula.

"Mkakati wa tano ni kuendelea kujenga mazingira rafiki na wezeshi ya usafirishaji wa mazao ya chakula na bidhaa zake kwenda nje ya nchi," alisema.

Aliwataka wananchi kuhifadhi chakula cha kutosha katika kaya zao pamoja kutumia mazao ya chakula kilichopatikana vizuri kutumika hadi kufikia msimu mwingine wa uzalishaji.

"Aidha, wakulima waliopata chakula cha ziada wanashauriwa wasiharakishe kuuza mazao yao mapema bali wasubiri hadi bei zitakapokuwa nzuri ndipo wauze na kwa wale waliopata utoshelevu kidogo wa chakula watumie vizuri mazao hayo kwa ajili ya chakula na si vinginevyo," alisema.

Hasunga aliwahimiza kufuatilia kwa karibu taarifa za mwelekeo wa mvua unaotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ili kuzitumia mvua hizo vizuri katika uzalishaji wa mazao.



# Makada 179 wapeta uteuzi udiwani CCM

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimetangaza majina ya watiania walioteuliwa kukiwakilisha chama hicho kuwania udiwani katika kata zote 179 za mkoa huo, huku kikitamba kuwa kimejiandaa kupata ushindi mkubwa.

Katibu Mwenezi wa chama hicho Mkoa wa Mbeya, Bashiru Madodi, aliwaambia waandishi wa habari mjini hapa juzi kuwa wanachama 1,181 walijitokeza kuomba kuteuliwa kugombea nafasi hizo katika wilaya zote sita za mkoa huo.

Alisema chama kwa kufuata kanuni na sheria zake, kilifuata michakato mbalimbali na kufikia uamuzi wa kuwateua wanachama hao 179 ambao ndiyo watapeperusha bendera ya chama hicho.

Madodi alitoa ufafanuzi kuwa katika Jimbo la Mbeya Vijijini lenye kata 28, walijitokeza wagombea 162,

**Sasa hivi tunawataka wana CCM walioteuliwa kuhakikisha wanaenda kuchukua fomu za kugombea katika ofisi husika na kuzijaza haraka iwezekanavyo ili zirejeshwe kabla ya Agosti 25 mwaka huu.**

Wilaya ya Kyela yenye kata 33 wagombea walikuwa 227 na Wilaya ya Chunya yenye kata 20 ilikuwa imevutia makada 105.

Madodi alibainisha kuwa katika Wilaya ya Mbarali yenye kata 20, walijitokeza wanachama 127, Wilaya ya Rungwe yenye kata 29 walijitosa makada 160, Jimbo la Busokelo lenye Kata 13 waliojitokeza walikuwa 83 na katika Jimbo la Mbeya Mjini lenye kata 36 walijitokeza wagombea 317.

"Sasa hivi tunawataka wana CCM walioteuliwa kuhakikisha wanaenda kuchukua fomu za kugombea katika ofisi husika na kuzijaza haraka iwezekanavyo ili zirejeshwe kabla ya Agosti 25 mwaka huu," alisema Madodi.

Alisema chama hicho kitawasimamia wagombea wake wakati wa kujaza fomu hizo, ili kuhakikisha wanazijaza kwa usahihi na kuzirejesha kwa wakati kuepuka kutokea matatizo.

Alisema chama hicho kimejiandaa kisaikolojia kuhakikisha kinafanya vizuri kwenye uchaguzi huo na kwamba kinaendelea kuwahamasisha wanachama wake ili kuhakikisha wanakuwa kitu kimoja wakati wa uchaguzi.

Madodi alisema chama hicho kimeendelea kufanya marekebisho ya maeneo yote ambayo kilikuwa kinafanya makosa na kusababisha kushindwa kwenye uchaguzi wa miaka iliyopita.

Alisema moja kati ya maeneo ambayo yalikuwa yanakikosesha ushindi chama hicho kwenye uchaguzi uliopita ukiwamo wa mwaka 2015 ambao kiliambulia kata 10 kati ya 36 za Mbeya Mjini, ni kuruhusu wasaliti kupenya ndani ya chama hicho na wakishaingia walikuwa wanashawishi watu wawachague wagombea wa upinzani.

Katika orodha ya wateule iliyotolewa juzi, Nipashe imebaini kupenya kwa idadi kubwa ya makada wapya wa CCM waliokuwa madiwani wa kupitia CHADEMA ambao walitimkia ndani ya CCM hasa katika Jiji la Mbeya, akiwamo aliyekuwa Meya wa Jiji la Mbeya, Mchungaji David Mwashilindi.



Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI), Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Dk. Edwin Chang'a (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, kituoni hapo hivi karibuni, kuhusu namna ya uandaaji na uhifadhi wa malisho bora ya mifugo kwa ajili ya kukabiliana na uhaba wa malisho wakati wa kiangazi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wafugaji wa Mbarali washauriwa machungio

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAFUGAJI katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameshauriwa kununua ardhi kwa ajili ya kuchungia mifugo yao badala ya kutegemea maeneo yaliyotengwa na serikali ili kuondokana na migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipokuwa akizungumza na wafugaji na wakulima wa Kata ya Imalilo - Songwe alipofanya ziara ya kusikiliza kero zinazowakabili ikiwamo migogoro ya ardhi.

Aliwataka wafugaji hao kuacha tabia ya kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima na kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, matukio ambayo yanasababisha migogoro ya mara kwa mara yakiwamo mapigano miongoni mwao.

Alisema maeneo yaliyotengwa na serikali hayatoshelezi mahitaji kutokana na baadhi ya wafugaji kufuga mifugo mingi, hivyo kufanya maeneo yaliyotengwa na serikali kutokidhi mahitaji.

"Hoja yangu ni kwamba wewe mfugaji ambaye umeamua kufuga mifugo mingi, muanze kununua ardhi yenu ili majani yanapokauka ama kuisha kwenye maeneo yaliyotengwa na serikali muyatumie maeneo yenu," alisema Chalamila.

Awali baadhi ya wafugaji walimweleza Chalamila matatizo yanayowakabili ukiwamo uhaba wa maeneo ya kuchungia, huku wakiomba serikali kulifuta Tangazo lake namba 28 la mwaka 2008 (GN 28) ambalo lilipanua Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, hivyo kupunguza maeneo ya kuchungia.

Mmoja wa wafugaji hao, Shaban Olelenganganu, ambaye ni mfugaji wa Kijiji cha Mwanavala, alisema kijiji hicho kina eneo la wafugaji ambalo lilipimwa wakati wa uwekaji wa matumizi bora ya ardhi lakini limevamiwa na wakulima.

# Wajasiriamali wakunwa ujenzi viwanda vya TPSF

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAJASIRIAMALI wasindikaji wa mazao ya chakula mkoani Mbeya, wamepongeza ujenzi wa viwanda vidogo jijini hapa kupitia mradi unaoratibiwa na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF).

Mradi huo unasimamiwa na Chama cha Wasindikaji wa Chakula na Mazao (TAFOPA) na kufadhiliwa na Shirika la Uswisi la HELVES.

HELVETAS imekuwa ikifadhili Mradi wa Kilimo Bora cha Mboga na Matunda kwa Wanawake na Vijana (KIBOWAVI) na kwa ushirikiano na TPSF, viwanda vidogo na mitambo ya baridi vinajengwa ili kurahisisha usafirishaji wa mazao yanayokubalika masoko katika masoko ya nje.

Renatus Lembileki, mmoja wa wajasiriamali hao, alisema wakulima wanaongeza uzalishaji wa mazao kwa sababu sasa wana sababu ya kufanya hivyo.

"Tuna matumaini makubwa sasa na tunaongeza uzalishaji wa mazao. Tatizo kubwa lilikuwa ni ardhi ya kujengwa viwanda, siyo fedha au mazao au wakulima, bali ardhi," alisema mtaalamu huyo wa kilimo mstaafu ambaye sasa analima kabichi na parachichi.

"Ni rahisi kupata fedha au kwingineko kwa muda mfupi ili kuanzisha viwanda, lakini bila ardhi utaviweka wapi? Hufiki kokote na hivi ndivyo imekuwa kwa muda mrefu.

"Balaa la ugonjwa wa corona limeibua masoka mengi yenye kuhitaji bidhaa za kilimo kati nchi za mashariki, kati, kusini mwa Afrika, Ulaya na Marekani, jamani watu huko wanahitaji mazao, siyo maneno," alisema.

Justin Fungo wa Glosama Bakers, alisema ujenzi wa viwanda hivyo unatoa uhakika kwa wajasiriamali wengi kupata sehemu za kuzalisha bidhaa zao na kupata masoko.

"Mradi huu utatuinua wengi kwani mtaji wa kununua mashine za kuchakata bidhaa umekuwa ni tatizo kubwa. Pia mradi utakuwa chachu ya kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa na kupunguza upotevu wa mazao kwa kukosa soko," alisema Fungo.

Syana Asalile wa Nuru Asili Farms, pia alisifu mradi huo na kusema utapunguza uharibifu wa mazao yao ya ufugaji na kilimo cha matunda kwa kuwa yatakuwa yanasindikwa jijini na kutafutiwa masoko ya ndani na nje ya nchi.

"Kwa muda mrefu nimekuwa ninachakata maziwa na ninatengeneza juisi za matunda, lakini bidhaa zetu zimekuwa zikiharibika. Mradi huu utakuwa mkombozi kwangu," alisifu Asalile.

Francko Jackson wa Jamii Kyela Products, pia alipongeza ufadhili wa HELVETAS na kusema utazalisha wajasiriamali wengi zaidi watakaojiajiri na kuongeza ubunifu katika kutengeneza bidhaa.

"Tatizo la uharibifu wa bidhaa lilionekana kama vile halina ufumbuzi. Kukamilika kwa mradi huu kutatufanya turasimishe bidhaa zetu kwenye mamlaka husika na kufanya bidhaa zetu zikubalike katika masoko ya ndani na nje," alisema.

Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, alipotakiwa kutoa maoni yake, alisema wanafuatilia kwa karibu mradi huo na kuongeza kwamba jitihada za uzoefu wao katika Jiji la Mbeya watazipeleka mikoa mingine.

# Tume yawaelekeza wasimamizi uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imewataka wasimamizi wa uchaguzi wa wilaya kuwa makini na kuvipitia vipengele vya Sheria ya Uchaguzi Namba Nne ya mwaka 2018 na kanuni za uchaguzi za mwaka 2020.

Sheria hiyo na kanuni zake, zitawapatia maelekezo mazuri ya kutekeleza majukumu yao katika kusimamia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Mabruk Jabu Makame, akizungumza wakati akifungua mafunzo kwa wasimamizi wa uchaguzi wa Zanzibar, alisema shughuli za uchaguzi mkuu zinahitaji kuendeshwa kwa kufuata misingi ya katiba, sheria na kanuni za uchaguzi ili kila mwenye haki aweze kuipata fursa hiyo.

"Waelekezeni vizuri juu ya utaratibu wa kisheria wateuliwa hao bila ya kujali ni nani amefika katika ofisi yako kupata huduma," alisema.

Alieleza kuwa licha ya kuwapo kwa mafanikio katika kuendesha kazi za uchaguzi katika hatua mbalimbali ikiwamo kazi ya mapitio ya majimbo ya uchaguzi, ambapo kwa sasa ni 50 badala ya 54.

Mengine ni uandikishaji wa wapigakura wapya na uhakiki wa taarifa za wapigakura, utoaji wa vitambulisho vya kupigia kura, lakini wanapaswa kuwa makini na waangalifu zaidi katika kazi ya utoaji wa fomu za uteuzi wa wagombea.

Aidha, aliwataka wasimamizi hao kuhakikisha wanafuatilia kwa ukaribu kazi ya upigaji kura, kuhesabu na kujumlisha kura katika vituo na majimbo wanayoyasimamia.

Naye Mkurugenzi wa Uchaguzi wa ZEC, Thabit Idarous Faina, alisema madhumuni ya Tume katika kuwapatia mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao katika uchaguzi mkuu 2020.

Akiwasilisha mada kuhusu kampeni za wagombea, Mkuu wa Kurugenzi ya Rasilimali Watu, Mipango na Uendeshaji wa ZEC, Saadun Ahmed Khamis, aliwataka wasimamizi hao wa uchaguzi wahakikishe mikutano yote ya kampeni za uchaguzi katika wilaya yake inaendeshwa katika muda na maeneo yaliyoainishwa kisheria.

# Jeshi la Polisi lamsaka mtuhumiwa wa mauaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja linamtafuta mtuhumiwa aliyefahamika kwa jina moja la Mahir anayetuhumiwa kutenda kosa la mauaji.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu matukio ya wiki Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Awadhi Juma Haji, alisema kuwa Agosti 14 mwaka huu majira ya saa 03:30 usiku katika maeneo ya Msikiti Swahaba Mtoni Kidatu, mtuhumiwa huyo alimchoma kisu sehemu ya kifuani upande wa kushoto Ibrahim Makame Saburi (20), na kusababisha kifo.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni Saburi kuamua ugomvi kati ya mtuhumiwa na Ramadhan Musa Mlekwa (16) katika sherehe za Maulid katika maeneo ya Mtoni Kidatu Mjini Unguja.

**Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi linaomba ushirikiano wa kupatiwa taarifa sahihi za mtuhumiwa huyo, ili kutiwa mbaroni.**

"Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi linaomba ushirikiano wa kupatiwa taarifa sahihi za mtuhumiwa huyo, ili kutiwa mbaroni," alisema Kamanda Awadhi.

Katika hatua nyingine, jeshi hilo linaendelea kufanya uchunguzi wa tukio la kujinyonga kwa Mohamed Abdalla Said (24), mkaazi wa Kimara Zanzibar.

"Ni kwamba mnamo tarehe 14/08/2020 majira ya saa 11:00 jioni katika maeneo ya Fuoni Kimara, Wilaya ya Magharibi "B", Mohammed Abdallah Said amekutwa akiwa amejinyonga chumbani kwake kwa kutumia shuka na kusababisha kifo chake," alisema kamanda huyo.

Alieleza kuwa mwili ulifikishwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa uchunguzi wa kidaktari na kukabidhiwa jamaa zake kwa mazishi.

Alisema taarifa za awali zinaeleza kuwa marehemu alikuwa na tatizo la ugonjwa wa akili.

Akizungumzia kuhusu ajali za barabarani, Kamanda Awadhi alisema katika mwendelezo wa operesheni za kukabiliana na vitendo vya uhalifu na wahalifu wa makosa mbalimbali yakiwamo ya usalama barabarani ili kudhibiti ajali, Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, limewakamata madereva 12 wa magari kwa makosa ya kubeba mizigo kwa njia ya hatari, kuzidisha mizigo, kuendesha magari mabovu na kuendesha gari akiwa amelewa.

Alimtaja dereva aliyekuwa ameendesha gari akiwa amelewa ni Fahm Ali Abdalla (27), mkazi wa Bububu.

"Ni tarehe 17/08/2020 majira ya saa 1:15 asubuhi maeneo ya Bububu katika barabara ya Bububu, dereva huyo alikamatwa akiwa anaendesha gari namba Z.309 GR aina ya ALTEZA na alipopimwa alikutwa na ulevi wa kiwango cha 114.23 mlg jambo ambalo ni kinyume na sheria," alisema.

Alisema pia wiki iliyopita walikamata waendesha vyombo vya moto vya maringi mawili (bodaboda) 20 kwa makosa ya kutovaa kofia ngumu, kuendesha bila leseni ya udereva.



Baadhi ya viongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na makandarasi wa majengo, wakiwa katika boti ya kusafiria kuelekea Kisiwa cha Kojani Pemba jana, kwa ajili ya kusaini fomu ya makabidhiano ya majengo ya maabara za sayansi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makabidhiano maabara za sayansi yaiva

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imesaini fomu ya makabidhiano ya majengo ya maabara za sayansi zilizopo Wilaya ya Wete Pemba baada ya kuridhishwa na matengenezo madogo waliyoyatoa hivi karibuni.

Utiaji wa saini huo umefanyika kati ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Idrisa Muslim Hija, msimamizi wa ujenzi na mshauri elekezi Isack Peter Kika na Meneja wa Mradi kutoka kampuni ya Home Africa, Shukuru Yassin Kavenuke.

Akizungumza katika hafla hiyo kisiwa cha Kojani Wilaya ya Wete Pemba, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Idrisa Muslim Hija, alisema katika kipindi cha mwezi mmoja walifika kwa ajili ya makabidhiano ya majengo hayo, lakini kutokana na kutokamilika kwa kiwango walichokubaliana hawakuweza kufanya hivyo na kuwataka kuyafanyia marekebisho ili yaweze kuwa katika hali ya ubora.

Aidha, Dk. Idrisa alimpongeza mkandarasi wa ujenzi huo kutokana na uvumilivu wao walioonyesha wakati wote wa ujenzi wa majengo hayo na kuwapo kutofautiana kati yao na wizara, na kuwa tofauti hizo lengo lake lilikuwa kuboresha ujenzi huo.

Alisema wizara itaendelea kutoa ushirikiano na makandarasi wa majengo yote katika miradi mbalimbali inayoianzisha ili mafanikio yazidi kupatikana katika sekta hiyo nchini.

Aliwataka wazazi na wananchi wote wa Wilaya ya Wete kuhakikisha wanashirikiana katika kuyalinda na kuyatunza majengo hayo ili yaweze kudumu kwa muda mrefu kwa faida yao na vizazi vijavyo.

Naye Naibu Katibu Mkuu Utawala na Uendeshaji wa wizara hiyo, Abdullah Mzee Abdullah, alisema ujenzi wa maabara hizo ni kutimiza ahadi za Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ya kutoa elimu bure, kuwa na majengo bora na ya kisasa na kulimaliza kabisa tatizo la ukosefu wa madawati katika shule mbalimbali.

Alisema ili nchi iendelee kuzalisha wataalamu wazalendo, ipo haja ya kuendelea kuimarisha elimu hasa masomo ya sayansi kwa kujenga maabara sehemu mbalimbali.

Mkuu wa Wilaya ya Wete, Mohamed Mussa Seif, aliishukuru Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuhakikisha maendeleo ya elimu yanapatikana katika visiwa vyote vya Unguja na Pemba.

Jumla ya maabara za sayansi tatu zilizojengwa na kampuni ya Home Afrika ziliopo Fundo, Kojani na Limbani zimekabidhiwa kwa wizara na kuwa kati ya maabara 22 zinazojengwa Unguja na Pemba kupitia mradi wa ZISP.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.

## NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA, Nyumba ya Gorofa 1, inauzwa na fremu za biashara, umeme na maji. Inafaa kwa kuishi na kwa biashara. Mawasiliano: 0757 079057.**

## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**Memory Nkhambule** anatangaza kupotea kwa Academic transcript chenye namba **2010-02-02644** kilichotolewa na Chuo Cha Muhimbili University of Health and Allied Sciences mwaka 2014. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MS/RB/7749/2017**

115863202

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Adili Sefu Humud** anatangaza kupotea kwa kadi ya Gari aina ya Grand Hiace yenye namba ya usajili **T256 CSD** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**REF/KAWE/2020**

115861902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Geofrey Rwehembiza Njumas** anatangaza kupotea kwa kadi ya Gari aina ya Pickup Hilux yenye namba ya usajili **T365 AKN** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**DAR/MAG/RB/596020/2020**

115863502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;233/2020**

**Ombi la PILI JUMA OCHIENG,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu JUMA OCHIENG OGOLA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 17/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/08/2020.

Tarehe 19/8/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU

115864402

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DORICE SIPERI KATTO** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri **T 368 DTS** aina yake **TOYOTA-IST.** Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa ktk kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi:
**MOR/MOR/RB/595771/2020.**

115864301

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Martin Assis Frank** anatangaza kupotea kwa kadi ya Gari aina ya **TOYOTA LAND CRUISER** yenye namba ya usajili **T371 ARX** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**DAR/SEL/591730/2020**

115864602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 213/2020**

**Ombi la BAHATI IBRAHIM BANDIMA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ISACK IBRAHIM BANDIMA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/08/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU

115865002

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Mali ajiuzulu, jeshi lachukua nchi

**BAMAKO,** Mali

RAIS wa Mali, Ibrahim Boubacar Keïta, jana, alitangaza kujiuzulu muda mfupi baada ya kuwekwa kizuizini na jeshi la nchi hiyo.

Akilihutubia Taifa kwa njia ya televisheni, Keïta alisema anaivunja serikali na bunge.

"Sitaki damu imwagike ili mimi kuendelea kubaki madarakani. Ikiwa leo, sehemu ya vikosi vilivyo na silaha wanataka hili liishe kwa kuingilia kati, nina cha kufanya?" Alisema Keïta.

Hatua ya Rais Keita kujiuzulu imekuja saa kadhaa baada ya kiongozi huyo wa juu na Waziri Mkuu, Boubou Cissé, kupelekwa kwenye kambi ya jeshi karibu na Mji Mkuu Bamako, hatua iliyosababisha mataifa ya Afrika Magharibi na Ufaransa kulaani kitendo hicho.

**Rais huyo pamoja na Waziri Mkuu wake walikamatwa na jeshi baada ya maandamano yaliyodumu kwa miezi kadhaa kumtaka kung'atuka madarakani.**

Rais huyo pamoja na Waziri Mkuu wake walikamatwa na jeshi baada ya maandamano yaliyodumu kwa miezi kadhaa kumtaka kung'atuka madarakani. Rais Keita ambaye alikuwa katika muhula wake wa pili wa uongozi alikuwa akituhumiwa kusababisha mdororo wa kiuchumi nchini humo pamoja na kushindwa kuyazuia makundi ya wapiganaji wa Kiislamu ambayo yameharibu amani ya nchi hiyo.

Awali msemaji wa serikali ya Mali, Yaya Sangaré alisema kwamba Rais wa nchi hiyo pamoja na Waziri Mkuu wamekamatwa na jeshi.

Sangaré ambaye ni msemaji wa serikali alisema Rais Ibrahim Boubakar Keita na Waziri Mkuu, Boubou Cisse, wapo katika mikono ya jeshi la nchi hiyo.

Hali hiyo inatajwa kwamba ni mwendelezo wa kile kilichoanza kama maandamano ambayo yamedumu kwa miezi kadhaa, kupinga utawala wa Rais Keita anayeshutumiwa kuisababishia nchi mdororo wa kiuchumi.

Wachambuzi wa masuala ya siasa wamelitaja tukio hili kuwa ni la mapinduzi.

Kukamatwa kwake kumewafurahisha maelfu ya waandamanaji ambao wamekuwa mitaani kila uchao kupinga utawala wake.

Katika maandamano mengine makubwa ya mwaka 2012, wapiganaji wa kiislam walilichukua eneo la Kaskazini mwa nchi hiyo, huku kukiendelea kuwa na ukosefu wa amani na kushuhudiwa mapigano baina ya jeshi na vikosi vya wapiganaji wa kiislam katika maeneo kadhaa nchini. **BBC**



Raia wa Mali wakiwashangilia wanajeshi, baada ya kumuondoa aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Ibrahim Boubacar Keita. **PICHA: REUTERS**

## Upinzani: EU msiutambue uchaguzi wa Belarus

**MINSK,** Belarus

KIONGOZI wa upinzani nchini Belarus, Sviatlana Tsikhanouskaya, jana alitoa wito kwa viongozi wa Umoja wa Ulaya (EU) kutoutambua uchaguzi wa urais uliompa ushindi kiongozi wa muda mrefu, Alexander Lukashenkona kuzusha maandamano makubwa ya kupinga utawala wake.

Katika ujumbe wa video aliotoa kuelekea mkutano wa dharura uliotishwa na EU kujadili hali nchini Belarus, Tsikhanouskaya aliwataka viongozi wa kanda hiyo, kuunga mkono vuguvugu la mageuzi kwenye Taifa hilo la uliokuwa muungano wa kisovieti.

Lukashenko ambaye amelitawala Taifa hilo la watu milioni 9.5 tangu 1994 alitangazwa mshindi kwa asilimia 80 katika uchaguzi wa Agosti 9, ambao upande wa upinzani ulisema uligubikwa na wizi wa kura.

Mapema wiki hii Tsikhanouskaya alisema yupo tayari kushika kwa muda wadhfa wa kiongozi wa kitaifa ili kuweza kuratibu marejeo ya uchaguzi.

Lakini washiriki wake walitangaza kile walichokiita baraza la uratibu kwa ajili ya kusaidia makabidhiano ya madaraka kwa amani.

Hata hivyo Lukashenko alirejea kwa mara kadhaa kukataa takwa la kujiuzulu na kupinga pia wazo la kufanya mazungumzo na upinzani, na kusema uratibu wa baraza kuwa ni sawa na jaribio la kuchukua madaraka. **DW**

## Biden kupambana na Trump

**WASHINGTON,** Marekani


CHAMA cha Democratic nchini Marekani kimempitisha, Joe Biden, kuwa mgombea urais. Huku kukiwa na hotuba za kusisimua kutoka kwa waliokuwa viongozi wa Taifa hilo.

Wagombea wawili waliokuwa marais wa Marekani kupitia chama hicho, Bill Clinton na Jimmy Carter, pamoja na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Colin Powell, wa Chama cha Republican, wamemuidhinisha rasmi Biden.

Clinton alisema ofisi ya Rais Donald Trump imesababisha vurugu katika Ikulu. Rais Trump alimpiku Biden katika kura ya maoni kabla ya uchaguzi wa Novemba.

Hii ni mara ya tatu kwa Biden kuingia kwenye kinyang'anyiro cha urais, huku mwakilishi huyo wa Chama cha Democratic akionekana kuwa katika kipindi cha mabadiliko makubwa, ikizingatiwa kwamba kampeni yake ilionekana kuwa katika hatari ya kudidimia mnamo Februari.

Usiku wa pili wa mkutano wa chama hicho, mada ikiwa ni masuala ya uongozi, Clinton alitoa hotuba iliyokonga mioyo ya wanachama waliohudhuria.



Trump Biden

"Donald Trump anasema tunaongoza duniani, sisi ndio nchi pekee iliyostawi kiuchumi ambayo kiwango cha waliokosa ajira imeongezeka mara tatu. Wakati kama huu, Ikulu inatakiwa kuwa kitovu cha kila kitu. Badala yake ni kituo cha dhoruba. Kinachopatikana huko ni fujo na ghasia pekee," alisema Clinton.

Kufuatia hotuba ya aliyekuwa mama wa kwanza wa Taifa hilo Michelle Obama na Seneta Bernie Sanders, hotuba zao zililenga kuonyesha wapiga kura namna chama cha Democratic ndiyo kilicho katika nafasi nzuri zaidi ya kurekebisha matatizo yaliyopo nyumbani na nje ya nchi.

Powell alisema Biden ana maadili niliyojifunza wakati ninakua huko South Bronn na nikiwa mwanajeshi.

Alisema kwamba anamuunga mkono kama rais kwa sababu inahitajika kurejesha maadili hayo katika Ikulu. Juni, Powell - ambaye alihudumu chini ya uongozi wa Rais George W Bush - alimtaja Rais Trump kama muongo na kumuidhinisha Biden.

Powell anajiunga na wanachama wengine wa Republican ambao wamemuidhinisha Biden. Usiku wa kwanza wa mkutano wa chama hicho, aliyekuwa Gavana wa Ohio, John Kasich, ni mmoja kati ya watu kadhaa waliojitolea kuunga mkono Chama cha Democrats.

Cindy McCain, mjane wa seneta wa chama cha Republican, John McCain, pia alitarajiwa kuzungumza kuhusu urafiki kati ya marehemu mume wake na Biden.

Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, John Kerry, pia alihudhuria mkutano huo kwa njia ya video na kukosoa uongozi wa Rais Trump.

Kerry aligusia uelewa wa Rais Trump wa masuala ya kidunia akisema anafahamu kwamba hakuna kinachoweza kutatuliwa bila kuunganisha Taifa. **BBC**

# DYBALA ANA FURAHA KUBAKI JUVE




**TURIN,** Italia

PAULO Dybala anafuraha pale Juventus na yupo kwenye mazungumzo na mabingwa hao wa Italia kuhusu mkataba mpya, kwa mujibu wa wakala wa mchezaji huyo, Jorge Antun.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alipewa tuzo ya mchezaji mwenye thamani zaidi Serie A msimu uliopita baada ya kufunga mabao 11 na kutoa pasi za mwisho sita wakati Juve wakishinda taji la tisa mfululizo la Scudetto.

Hata hivyo, taarifa za hivi karibuni za nchini Italia zimekuwa zikibainisha kwamba, Dybala anaweza kuondoka pale Turin kuelekea msimu ujao, huku Real Madrid wakitajwa kumuwania.

Wakala wa Dybala amekanusha taarifa hizo, na amesema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, anaweza kuongeza mkataba wake wa sasa hapo kwenye dimba la Allianz.

"Nimesoma uvumi huo kwenye magazeti siku za hivi karibuni - kwa uhakika kabisa ni za uzushi," alisema Antun, akinukuliwa na Calciomercato.

"Dybala ni mchezaji wa Juventus na ana furaha kubwa hapa.

"Tunafanya kazi na klabu kuhakikisha anasaini mkataba mpya na kuendelea na maandalizi ya kuelekea msimu mpya."

Dybala ametumia misimu mitano akiwa na Juventus na mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2022.

# Willian: Martinelli atakuwa bora EPL




**LONDON,** England

WILLIAN amempigia chapuo mchezaji kijana wa Arsenal, Gabriel Martinelli kuwa na uwezo wa kuja kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi kwenye Ligi Kuu ya England mara tu atakapopona kutoka majeraha ya muda mrefu.

Martinelli alijiunga na Arsenal akitokea klabu ya nchini Brazil ya Ituano mwaka jana na kufunga mabao 10 katika mechi 26 kabla ya kuumia goti la kushoto wakati wa mazoezi Juni.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye bado hajaitwa katika kikosi cha timu ya Taifa ya Brazil, alifanyiwa operesheni yenye mafanikio mwezi uliopita na anatarajiwa kurudi uwanjani mwishoni mwa mwaka huu 2020.

Licha ya mjeraha hayo ya Martinelli, mchezaji mwenzake mpya wa Arsenal, Willian anaona ana nafasi kubwa ya kuwa mchezaji bora wa EPL kutokana na kipaji chake.

"Ana nafasi kubwa katika siku zake za usoni, nafikiri hivyo," alisema Willian akiiambia tovuti ya Arsenal.

"Anaweza kuwa mmoja wa wachezaji bora kwenye Ligi Kuu ya England bila shaka yoyote.

"Kwa sababu ana ubora na kipaji cha hali ya juu na mara zote akicheza huwa anawavutia wengi dimbani. Hivyo naamini atakuwa bora sana siku za usoni."

Willian alijiunga na Arsenal wiki iliyopita baada ya kumaliza kipindi chake cha kucheza kule Chelsea na aliondoka kama mchezaji huru na amekwenda kujiunga na Mbrazil mwenzake, David Luiz.

# Wenger akana ukocha Uholanzi

**LONDON,** England

ARSENE Wenger amekanusha ripoti inayodai kwamba amepewa ofa ya kuwa kocha mpya wa timu ya Taifa ya Uholanzi.

Kocha huyo wa zamani wa Arsenal alidai kwamba amepewa ofa ya kuhudumu kama kocha wa Uholanzi, kwa mujibu wa Fox Sports, huku Ronald Koeman akitajwa kwenda kuwa kocha mpya wa Barcelona.

Wenger mwenye umri wa miaka 70, hajawa na timu tangu alipoondoka Arsenal mwaka 2018 na kwa sasa anafanya kazi kama Ofisa Mkuu wa Maendeleo ya Soka Duniani kwenye Shirikisho la Soka la Kimataifa, FIFA.

Mfaransa huyo amekanusha taarifa hizo kwa kuiambia De Telegraaf: "Huo ni uongo. Sijapata ofa yoyote kwa sasa.

"Mimi ndio pekee mwenye jukumu la kuzungumzia majaliwa yangu."

Wenger aliondoka Arsenal baada ya misimu 22 kwenye Ligi Kuu ya England, akishinda mataji matatu ya EPL na saba ya FA.

Koeman anatarajia kuchukua mikoba ya kuinoa Barcelona baada ya Quique Setien kufukuzwa kutokana na klabu hiyo kukosa taji lolote kwa msimu wa 2019-20 ikiwamo kutolewa kwa kipigo cha aibu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya robo fainali na Bayern Munich.



# Guardiola hawezi kuinoa Barca kwa sasa-Wakala

**BARCELONA,** Hispania

PEP Guardiola ana majukumu makubwa zaidi pale Manchester City na kurudi kwenye klabu yake ya zamani Barcelona "kwa sasa haiwezekani", kwa mujibu wa wakala wa kocha huyo kutoka Catalunya, Josep Maria Orobitg.

City kwa msimu wa tatu mfululizo imetolewa kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kuzusha uvumi juu ya majaliwa ya Guardiola pale kwenye dimba la Etihad.

Yupo katika mwaka wake wa mwisho katika mkataba wake, wakati Barca wamemtimua kocha wao, Quique Setien, na Guardiola ni mmoja anayetajwa kuchukua nafasi hiyo.

Hata hivyo, mwakilishi wa Guardiola, Orobitg amesisitiza kocha huyo mwenye umri wa miaka 49, ataheshimu mkataba wake na City.

"Ndio, Pep atabakia City kwa asilimia 100," alisema akiiambia Goal.

Guardiola ameshinda mataji 14 kwa misimu minne akiwa kule Barca, lakini Orobitg aliongeza "kwa sasa haiwezekani" kurudi kule Catalunya.

Barcelona walikumbana na kipigo cha aibu cha mabao 8-2 kutoka kwa Bayern Munich wiki iliyopita kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa sasa Ronald Koeman ambaye ni mlinzi wa zamani wa kikosi hicho, anatajwa kwamba ana nafasi kubwa ya kupewa mikoba ya ukocha pale Camp Nou.





# IBRAHIMOVIC ATASAINI MKATABA MPYA - PIOLI

**MILAN,** Italia

KOCHA Mkuu wa AC Milan, Stefano Pioli hana shaka na majaliwa ya Zlatan Ibrahimovic kwani anaamini atasaini mkataba mpya wa kubakia hapo kwenye Uwanja wa San Siro.

Ibrahimovic alirudi Milan akitokea klabu ya Ligi Kuu ya Marekani (MLS), LA Galaxy Januari kwa mkataba wa muda mfupi na baadaye akaisaidia vizuri timu hiyo na kunusuru kibarua cha Pioli.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, alifunga mabao 10 katika mechi 18 alizocheza, na kuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kufikisha mabao hayo kwenye historia ya Serie A.

Katika mahojiano na kampuni inayoidhamini Milan, Skrill, Pioli alielezea mchango wa Ibrahimovic kwa kukisaidia kikosi hicho msimu huu.

"Zlatan ni mchezaji mwenye weledi," alisema. "Anawafundisha wachezaji vijana, ni nguzo kwa wachezaji wenzake kwenye timu na anaheshimiwa sana.

"Siri yake kubwa ni kwamba, mara zote anataka kushinda na kujiimarisha yeye mwenyewe. "Mchango wake kwenye kikosi chetu umeonekana, hivyo nina imani kubwa atasaini kuongeza mkataba mpya na kuendelea kubakia hapa na kikosi hiki."

# Klopp kustaafu akiondoka Liver

**LIVERPOOL,** Hispania

JURGEN Klopp anafikiria kuondoka Liverpool wakati mkataba wake utakapomalizika na anaweza kustaafu kazi ya ukocha kwa muda wa mwaka mmoja.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 53, ameshinda taji la Ligi Kuu ya England, Ligi ya Mabingwa Ulaya, Klabu Bingwa Dunia na UEFA Super katika misimu mitano aliyokaa pale kwenye dimba la Anfield wakati huu mkataba wake ukitarajiwa kumalizika mwaka 2024.

Klopp alisaidia Liverpool kumaliza ukame wa miaka 30 wa kutoshinda taji la Ligi Kuu, lakini hatasaini mkataba mpya akiondoka kwa miamba hao.

"Nitachukua mwaka mmoja nje ya soka na nitajiuliza mwenyewe kama nitalimisi soka. Kama nikisema hapana, huo ndio utakuwa mwisho wa kazi ya ukocha kwa Jurgen Klopp," alisema akiiambia Sport Buzzer.

"Kama siku moja sitakuwa tena kocha, ni kitu kimoja ndio nitakimisi: Ule muda w a tahayari kabla ya mchezo.

"Mawazo yanakuwa mengi kabla ya mchezo na unakuwa na mbinu nyingi kichwani, lakini kuna wakati mambo yanageuka na kwenda tofauti kabisa na matarajio yako."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KYLIAN MBAPPE: NEYMAR ANASTAHILI BALLON D'OR

## Nina uhakika kama tukishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, anaweza kushinda...

**LISBON,** Ureno

KYLIAN Mbappe anaamini Neymar anaweza kuwa na thamani ya kushinda tuzo ya Ballon d'Or kama ataisaidia Paris Saint-Germain kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**Tuzo hiyo kwa mwaka huu 2020 haitatolewa kwa sababu ya athari za mlipuko wa virusi vya corona uliotingisha ulimwengu wa soka.**

Hata hivyo, Neymar alionyesha kiwango cha juu wakati PSG ikiibuka na ushindi mzuri wa mabao 3-0 dhidi ya RB Leipzig kwenye hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumanne.

Kama wataweza kulibeba taji hilo, Mbappe anaamini mchezaji mwenzake huyo anaweza kuwa na matumaini makubwa ya kutajwa kuwa mchezaji bora duniani.

"Nina uhakika kama tukishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, anaweza kushinda Ballon d'Or," alisema Mbappe akiwaambia waandishi wa habari mjini Lisbon.

"Angependa kushinda na ninapenda ikiwa hivyo, na hilo litawezekana tu kama tukishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya."

Mbappe na Neymar walicheza kwa upatina mzuri, ingawa alisaidiwa na mshambuliaji wa tatu wa PSG kati ya watatu wa mbele, Angel Di Maria, kufunga bao na alitoa pasi za mwisho mbili.

"Kocha wetu anasema tunaelewana kila mmoja tukiwa uwanjani," alisema Mbappe. "Ni muhimu kwa timu yote.

"Kwa kweli inaleta raha kucheza pamoja na mchezaji kama Neymar. Ni mmoja wa wachezaji bora duniani na amethibitisha hilo. "Hakufunga, lakini si jambo la muhimu. Badala yake Di Maria ndio alinufaika."

Mbappe alianza kwa kushinda Kombe la Dunia na Ufaransa mwaka 2018 nchini Urusi na anaamini sasa wanaweza kuwa na mafanikio kama hayo mjini Lisbon.

"Nikiwa mkweli, mafanikio haya yanaweza kuwa kama yale tuliyoyapata kule Urusi kama tukifanikiwa kubeba taji. "Naamini tutakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuisaidia PSG kubeba taji hili.

"Ni bahati kubwa kwangu kwamba nilishinda Kombe la Dunia, na sasa naweza kushinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL YAMUWANIA GABRIEL

ARSENAL ina matumaini ya kukamilisha makubaliano ya pauni milioni 22 kumsajili mlinzi wa Lille, Gabriel Magalhaes, 22. Everton na Napoli pia nazo zinamnyatia mchezaji huyo wa Brazil. ***(ESPN)***

### CHELSEA PAZURI KWA KAI

CHELSEA itakamilisha makubaliano ya mchezaji wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz,21, ndani ya siku 10 zijazo. Raia huyo wa Ujerumani anataka kuhakikishiwa makubaliano ya miaka mitano. ***(Bild, via Express)***

### DYBALA, POGBA KUPISHANA

JUVENTUS huenda ikamtumia mshambuliaji, Paulo Dybala, 26, kama sehemu ya makubaliano ya mabadilishano na Manchester United, ili kumrejesha Paul Pogba katika Ligi ya Serie A. Raia huyo wa Argentina, Dybala amebakiwa na miaka miwili kule Turin.

### COSTA NDANI RADA UNITED

MANCHESTER United wanamfuatilia kwa karibu zaidi winga wa Juventus na Brazil, Douglas Costa mwenye umri wa miaka 29. ***(Sky Sports)***

### WATFORD YAIKATALIA EVERTON

KLABU ya Watford imekataa kitita cha kwanza kutoka Everton kwa ajili ya kiungo wa kati, Abdoulaye Doucoure mwenye umri wa miaka 27. Hornets inataka pauni milioni 25 kwa mchezaji huyo raia wa Ufaransa. ***(Standard)***

### LAZIO YAMTAKA ENDERSON

LAZIO inafikiria kumsajili kiungo wa kati wa West Ham na Brazil, Felipe Anderson mwenye umri wa miaka 27, baada ya David Silva kuwatosa dakika za mwisho na kwenda Real Sociedad ya Hispania. ***(Star)***

### BURNLEY YAMUWANIA BAPTISTE

KLABU ya Burnley inafanya mazungumzo ya kutaka kumsajili kiungo wa Angers, Mfaransa Baptiste Santamaria mwenye umri wa miaka 25. ***(RMC Sport, via Daily Mail)***

### BRIGHTON KUBAKISHA NYOTA

BRIGHTON imesema nahodha wake, Lewis Dunk mwenye umri wa miaka 28 na mlinzi Ben White mwenye miaka 22, watabaki katika klabu hiyo. Dunk amehusishwa na Chelsea huku Leeds ikitaka kufanya mazungumzo na White. ***(Talksport)***

### DOUGLAS KUSEPA EVERTON

KLABU ya Aston Villa ina imani kubwa ya kuendelea kuwa na kiungo wa kati, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 22. Raia huyo wa Brazil alikuwa amehusishwa na kurejea Manchester City. ***(Express and Star)***

### HENDERSON KUFUNGWA SEFFIELD

SHEFFIELD United inafikiria kutoa ofa nyingine ya mkopo kwa mlinda mlango wa Manchester United, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 23 raia wa Uingereza. ***(ESPN)***

### SOUTHAMPTON KWA MCKENNIE

KLABU ya Southampton inafanya mazungumzo na Schalke juu ya makubaliano ya pauni milioni 20 kwa ajili ya kumsajili kiungo wa kati raia wa Marekani, Weston McKennie mwenye umri wa miaka 21. ***(Sky Sports)***

**HABARI MICHEZO**

## Dante amwaga wino KMC FC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC FC, imeingia rasmi kwenye vita ya kuwania wachezaji kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, baada ya kumsajili beki wa Yanga aliyemaliza mkataba na klabu hiyo, Andrew Vicent 'Dante' kwa muda wa mwaka mmoja.

Usajili huo ulifanywa juzi jioni na sasa Dante ni mchezaji halali wa klabu hiyo ambayo inafanya iwe na wachezaji wawili wapya ambao imewatambulisha.

Mtandao rasmi wa klabu hiyo, baada ya kumsainisha na kuchapisha picha ya mchezaji huyo akisaini, ulisindikizwa na ujumbe "uzoefu na weledi na vitu muhimu sana kwenye kazi yoyote ile. Andrew Vicent 'Dante', rasmi Kinoboy. Amesaini mkataba wa mwaka mmoja akitokea Yanga."

Mbali na Dante, klabu hiyo pia imesainisha beki wa kati wa Lipuli, David Mwasa ambaye ameingia mkataba wa miaka miwili kuitumikia klabu hiyo.

Dante alisajiliwa na Yanga akitokea Mtibwa Sugar mwaka 2016 na kudumu kwa misimu yote hiyo, ingawa kwa siku za karibuni alikuwa na mgogoro na viongozi wa klabu hiyo kiasi cha kususa na kukaa nyumbani, kabla ya kurejeshwa tena na kuendelea na kazi kama kawaida.

## Lusajo, Balora sasa njiapanda Namungo

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA tegemeo wa klabu ya Namungo, Reliatns Lusajo na kipa namba moja wa klabu hiyo ni kati ya wachezaji waliomaliza mikataba yao kwenye klabu hiyo, hivyo kwa sasa wana uwezo wa kujiunga na klabu yoyote ile.

Taarifa iliyochapishwa kwenye mtandao rasmi wa klabu hiyo ni kwamba wachezaji hao wamemaliza mikataba yao. Ingawa mtandao huo haujaweka wazi kama inaweza kukaa nao na kuwaongeza mipya, lakini wachezaji hao kwa sasa wako huru kufanya mazungumzo na klabu yoyote ikiwamo Namungo yenyewe.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Hassan Zidadu, mapema wiki hii alisema moja kati ya usajili watakaoufanya ni wa golikipa, hivyo Balora ana nafasi finyu ya kubaki kwenye klabu hiyo.

Mbali na wachezaji hao, mwingine aliyemaliza mkataba ni George Makang'a, mchezaji aliyesajiliwa na klabu hiyo akitokea Biashara United.

Wengine ni John Mbise, John Kelvin, mchezaji wa zamani wa Simba na Mbao FC, Jamal Mwambeleko, Jukumu Kibanda na Adam Oseja.

# WAZIRI MKUU MGENI RASMI AZAM FESTIVAL

**Na Saada Akida**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, Jumapili atakuwa mgeni rasmi katika kilele cha Wiki ya Chamazi 'Azam Festival', huku 'Wanalambalamba' hao wakicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Namungo FC, itakayopigwa Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zakaria 'Zaka Zakazi', alisema uongozi wa klabu hiyo umemwomba Waziri Mkuu kuwa mgeni rasmi na tayari amethibitisha mwaliko huo, ambapo pia atashuhudia mechi hiyo watakayoitumia kutambulisha wachezaji wao wa msimu ujao pamoja na jezi.

Alisema wamelazimika kucheza na Namungo FC, baada ya kukosa timu kutoka nje ya nchini husussan Zambia na Burundi walikopeleka maombi.

**"Tulikuwa na mawasiliano na baadhi ya timu kutoka Zambia na Burundi, ambao ligi zao zimemalizika hivi karibuni, tulipata timu moja ya Zambia, lakini kutokana na sababu zilizopo nje ya uwezo wetu, walitujulisha mapema kwamba hawatakuja kwa matatizo yao binafsi," alisema Zakazi.**

Alisema kwa Burundi timu ambayo walizungumza nayo pia ilitoa sababu nje ya uwezo wao, hivyo kuamua kuialika Namungo ya Lindi.

"Mbali na nchi hizo, tumeshindwa kufanya mazungumzo na mataifa mengine kwani ligi zao zilisimama na kushindwa kuendelea kutokana na janga la virusi vya corona na mipaka yao bado imefungwa," alisema Zakazi na kuongeza.

"Huu ni mwaka wetu wa kwanza kuandaa tamasha hili likiwa na lengo la kutambulisha wachezaji pamoja na jezi za msimu mpya, lakini pia kuwafanya watu na mashabiki wa soka Kata ya Chamazi, Mbande na Wilaya ya Temeke kwa ujumla kuwahamasisha kupenda kujitokeza uwanjani kuisapoti timu yao inapocheza Chamazi."

**IMEWADIA...**




Ofisa Habari wa Klabu ya Simba, Haji Manara, akizungumza na waandishi wa habari za michezo jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza mchezo wao wa kirafiki wa Simba Day dhidi ya Vital'O ya Burundi utakaochezwa Jumamosi wiki hii, katika Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam. Kulia ni mwakilishi wa serikali kutoka Kituo cha Taifa kinachohusika na kuratibu malipo kwa njia ya mtandao (National Data Center), watakaohusika kuuza kadi maalum za kuingilia uwanjani, Mwanasha Semboko. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Yondani kuibukia JKT Tanzania*

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya JKT Tanzania upo katika mazungumzo na beki wa zamani wa Yanga, Kelvin Yondani kwa ajili ya kuingia naye mkataba wa kuitumikia timu yao hiyo kwa msimu wa 2020/21 wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Makamu Mwenyekiti wa timu hiyo, Thabiti Baraji, alisema wamepokea mapendekezo ya benchi lao la ufundi kwa kuutaka uongozi kuzungumza na beki huyo ili kwenda kuimarisha ukuta wa timu hiyo.

"Tulimtumia mchezaji wetu Mwinyi Kazimoto kumfikishia ujumbe wetu, pia kutaka kujua kama amesaini timu yoyote, tulipata majibu mazuri na juzi usiku nimeongea na mchezaji huyo na tunatarajia kati ya siku hizi mbili kukutana naye kwa ajili ya kuweka ofa mezani," alisema Baraji.

Alisema pande hizo mbili kila mmoja atasikiliza ofa ya mwenzake na ana imani wataenda sawa kwa sababu wanahitaji huduma ya beki huyo mwenye uzoefu mkubwa kutokana na kucheza muda mrefu.

"Tunapambana kuhakikisha tunaafikiana na Yondani ili msimu huu mpya kucheza ndani ya timu yetu, nina imani kila kitu kitaenda vizuri na kufanikiwa kupata saini ya beki huyo," alisema Baraji.

Alisema licha ya kuendelea na mchakato wa usajili, kikosi chao tayari kimeanza mazoezi kwenye viwanja vya Mlalakuwa jijini Dar es Salaam kujiandaa na Ligi Kuu Tanzania Bara inatakayoanza kutimua vumbi Septemba 6, mwaka huu.

Yondani kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake na Yanga, ambayo walishindwana katika maslahi wakati wa mazungumzo ya mkataba mpya.

Kwa mujibu wa ratiba ya ligi hiyo, Septemba 6, JKT Tanzania watakuwa ugenini katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba kuvaana na Kagera Sugar.

# Micheze

Alhamisi Agosti 20, 2020

Nipashe




Mbappe: Neymar anastahili Ballon d'Or

UKURASA 22

IMEISHA HIYO...




Angel Di Maria akishangilia na Neymar (kulia), baada ya kufunga bao moja na kutoa pasi za mwisho mbili katika ushindi wa 3-0 Paris Saint-Germain iliyoupata dhidi ya RB Leipzig ya Ujerumani kwenye mechi ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, iliyopigwa Jumanne usiku katika Uwanja wa Luz Jijini Lisbon, Ureno. PSG sasa fainali itakutana na mshindi wa jana usiku kati ya Olympique Lyon ya Ufaransa na Bayern Munich ya Ujerumani. **PICHA: MTANDAO**

## Mukoko, Kisinda ni kishindo Yanga leo



**Na Faustine Feliciane**

KISHINDO kikubwa kinatarajiwa kusikika kuanzia Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere hadi mitaa ya Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam wakati Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM, Injinia Hersi Said, wanaoidhamini Klabu ya Yanga atakapotua leo majira ya 7:20 mchana na viungo fundi wawili kutoka DR Congo.

Hersi amekamilisha usajili wa kiungo mkabaji Mukoko Tonombe na winga Tuisila Kisinda kutoka Klabu ya AS Vita ya DR Congo, na leo nyota hao watatua tayari kujiunga na kikosi hicho kinachoendelea na mazoezi katika Uwanja wa Chuo cha Sheria jijini Dar es Salaam chini ya makocha wasaidizi, Riedoh Berdien na Said Maulid. Meneja wa Klabu ya Yanga, Hafidh Saleh, aliliambia Nipashe jana kuwa nyota hao watawasili Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere na kupokelewa na viongozi wa klabu hiyo.

"Suala la maandalizi ya mapokezi na hamasa ya kuwapokea jambo hilo lipo mikononi mwa akina Nugaz [Antonio], ila taarifa tuliyonayo wanawasili kesho mchana," alisema Hafidh.

Kuhusu Kocha Mkuu, alisema: "Hili jambo la kocha lipo kwa viongozi, wa juu ndio wanaweza wakalizungumzia zaidi, kwa sasa bado makocha waliopo ndio wanasimamia mazoezi na yanaendelea vizuri."

Hata hivyo, licha ya Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz, kutopatikana jana, taarifa zilizolifikia Nipashe ni kwamba yameandaliwa mapokezi ya kishindo watakapotua nyota hao leo.

# Bwalya aiona Chipolopolo Simba

**Na Mwandishi Wetu**

### Asema kombinesheni yake na Chama kama wakiwa timu ya Taifa ya Zambia, kuwaona Simba Day shilingi....

HUKU akiwa ameanza kujifua na kikosi cha Simba katika Uwanja wa Mo Simba Arena, Bunju jijini Dar es Salaam, kiungo mpya wa klabu ya Simba, Larry Bwalya amesema amefurahi kujiunga na miamba hiyo ambayo sasa itamkutanisha katika klabu moja na Clatous Chama kama ilivyo kwenye timu ya Taifa ya Zambia 'Chipolopolo'.

**Bwalya ambaye amejiunga na Simba katika dirisha hili la usajili akitokea Lusaka Dynamos ya Zambia, timu ya zamani ya Chama, amesema amefurahi kumkuta kiungo mshambuliaji huyo ndani ya Simba na anaamini watacheza vizuri na kuisaidia timu hiyo kupata mafanikio wakishirikiana na nyota wengine.**

Wawili hao wanaichezea Chipolopolo, jambo ambalo linamfanya Bwalya kueleza kuwa watatengeneza maelewano makubwa wakishirikiana na wachezaji wengine ndani ya kikosi cha Simba.

Bwalya ambaye anaweza kucheza nafasi zote za safu ya kiungo wa ulinzi na ushambuliaji kwa ufasaha, alisema jijini juzi kuwa baada ya kupokea ofa ya klabu hiyo hakufikiria mara mbili kuikubali kwa kuwa Simba ni timu yenye historia kubwa na amependa kuwa sehemu ya historia hiyo.

Hata hivyo, amewaomba mashabiki kuendelea kutoa sapoti kwa wachezaji na kujitokeza kwa wingi uwanjani kila timu yao inapocheza ili kuongeza morali kitu ambacho kitachangia kupatikana matokeo.

"Nimefurahi kucheza pamoja na Chama kwenye timu moja kama ilivyo timu ya Taifa. Ninaamini kwa pamoja tutafanya vizuri pamoja na wachezaji wengine kwa ajili ya kuisaidia timu kupata ushindi.

"Simba ni klabu yenye historia kubwa na ninapenda kuwa sehemu ya historia hiyo, kikubwa tunaomba mashabiki waendelee kutusapoti tunaamini tutafanya vizuri," alisema Bwalya akizungumza na tovuti ya klabu hiyo.

Hata hivyo, Bwalya bado hajakutana rasmi na Chama mazoezini, kutokana na kiungo huyo anayewakuna mashabiki wa Simba, kuwa nyumbani kwa mapumziko mafupi, wakati huu akitarajiwa kurejea leo.

Mashabiki wa Simba wataanza kumshuhudia Bwalya Uwanja wa Mkapa Jumamosi pamoja na nyota wengine waliosajiliwa msimu huu watakaposhuka dimbani katika Tamasha la Simba Day kuivaa Vital'O ya Burundi.

Mbali na Bwalya, wachezaji wengine wapya watakaotambulishwa Jumamosi ni Ibrahim Ally Ame kutoka Coastal Union, Charles Ilamfya (KMC), David Kameta (Lipuli FC), Chriss Mugalu (Lusaka Dynamos), Joash Onyango (huru) aliyemaliza mkataba na Gor Mahia ya Kenya na Benard Morrison (huru) baada ya kumaliza mkataba na Yanga.

Baada ya mechi hiyo, kituo kitakachofuata kwa Simba kitakuwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha tayari kwa mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Namungo FC utakaopigwa Agosti 30.

Mchezo huo utakuwa maalum kwa ajili ya kukaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu Bara unaotarajiwa kuanza Septemba 6, mwaka huu, huku mabingwa watetezi hao wakifungua dhidi ya Ihefu FC mechi ambayo itapigwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Katika hatua nyingine, Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, jana alitangaza viingilio vya mechi ya Jumamosi dhidi ya Vital'O, vitakuwa Sh. 2,000 kwa Uwanja wa Uhuru huku Uwanja wa Mkapa vikiwa, Sh. 7,000 mzunguko, VIP C Sh. 20,000 wakati VIP B ikiwa Sh. 30,000 huku VIP A akisema ni Sh. 40,000 na kwa tiketi za Platinum zikipatikana kwa Sh. 150,000 tu.

"Kwa wale mashabiki watakaonunua tiketi ya Platinum watapewa usafiri kutoka Serena hadi uwanjani msafara ukiongozwa na polisi huku wakipewa chakula pamoja na vinywaji wakati mchezo ukiendelea, lakini watapewa kadi ya kuingia kwenye pati baada ya mechi itayofanyika Elements," alisema Manara.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >